

Hadithi ya Maisha Yangu

Los Angeles, California, USA

Aprili 19, 1959

1 Hebu na tuinamishe vichwa vyetu kwa muda kidogo tu kwa ajili ya maombi.

Baba yetu wa Mbinguni mwenye neema, kwa kweli ni kwa majaliwa tuliyonayo ya kukuendea Wewe, Mungu na Mwokozi wetu. Kusikia wimbo huu wa ajabu, Jinsi Wewe Ulivyo Mkuu, inatufurahisha kwa sababu tunajua ya kwamba Wewe ni mkuu. Nasi tunaomba ya kwamba ukuu Wako utadhihirishwa kwetu upya, alasiri ya leo, tunaponena. Nami nimeangukia, kwa mara ya kwanza katika miaka mingi, kujaribu kurudi katika maisha ya zamani, nami ninaomba ya kwamba utanipa nguvu na—na kile ninachohitaji, Bwana, kuwa katika saa hii. Na jalia makosa yangu yote maishani yawe tu jiwe la kukanyaga kwa wengine, ambalo lingewaleta karibu na Wewe. Tujalie, Bwana. Jalia wenye dhambi wazione nyayo kwenye mchanga wa wakati, na jalia waongozwe Kwako. Mambo haya tunaomba katika Jina la Bwana Yesu. Amina.

Mnaweza kuketi.

2 [Ndugu Glover anasema, "Unaweza kuomba lesu hizi kabla hujaanza?" — Mh.] Nitafurahi. ["Kuna hizo na hizi za kuomba."] Vema, bwana, asante. Kama vile mtu huyu mtakatifu, Ndugu Glover, ambaye nimemjua sasa kwa miaka kadhaa, nilikuwa na majaliwa ya kuwa pamoja naye kitambo jana jioni. Naye ameniambia ... alikuwa hawezi kwa kitambo kidogo, akipumzika. Na sasa, akiwa na umri wa miaka sabini na mitano, anarudi katika utumishi wa Bwana. Mimi sijafikia nusu ya uchovu kama nilivyokuwa kabla ya kusikia jambo hilo. Nilifikiri nilikuwa nimechoka, bali si—siamini nimechoka. Hivi punde alikuwa ameniwekea hapa lesu kadhaa, katika—namna ya bahasha, na kadhalika, ambazo ziko ndani na tayari zimefungwa.

3 Sasa, ye yote wenu katika redio, ama hapa, anayetaka moja ya lesu hizi, nanyi mnge ... Angelus Temple huzituma kila mara, wakati wote. Ungeweza kuwaandikia hapa Angelus Temple na wao wataiombea, kwa sababu nitakuhakikishia kwamba ni Maandiko. Ni ahadi ya Mungu.

Na kama ingekuwa kwamba mnetaka niwaombe mmoja, mbona, nitafurahi kufanya hivyo. Ingekupasa tu kuniandikia kwa sanduku la posta 3-2-5, 325, Jeffersonville, huendelezwa J-e-f-f-e-r-s-o-n-v-i, I mbili, e. Jeffersonville, Indiana. Ama kama huwezi kufikiria juu ya sanduku la posta, andika tu "Jeffersonville." Ni mji mdogo, wenye watu kama thelathini na tano elfu. Kila mtu ananijua kule. Na kwa hiyo tungefurahia kuomba lesu na kuwatumia.

4 Na, sasa, tumekuwa na mafanikio makubwa katika kufanya jambo hili, kwa sababu ... Utapata barua ndogo ikiambatana nayo, kwamba watu ulimwenguni pote huomba kila asubuhi saa tatu, na saa sita, na saa tisa. Nawe unaweza kufikiria, huko upande wa pili wa ulimwenguni, inawabidi kuamka saa ngapi usiku kufanya maombi haya. Kwa hiyo iwapo hawa wote makumi elfu, na mara elfu, wanapeleka maombi kwa Mungu wakati huo huo kwa ajili ya huduma hii, ugonjwa wako, Mungu hawezi kukataa hilo. Na kwa hiyo sasa sisi, kama nisemavyo, hatuna mipango yo yote, hatutaki hata senti moja ya fedha. Tunaninii tu ... Kama tunaweza kukusaidia, hiyo ndiyo sababu tuko hapa. Na hebu sisi ...

Mtu fulani analeta lundo lingine la lesu.

5 Sasa, kama huna lesu uliyotaka kutuma, vema, basi andika tu, hata hivyo. Kama huihitaji sasa hivi iweke katika kitabu cha Matendo, katika Biblia, sura ya 19. Na itakuwa namna ya utepe mdogo mweupe ambao utatumwa kwako, na maelezo jinsi ya kuungama dhambi zako kwanza. Na (asante) jinsi ya kuungama dhambi zako. Hupaswi kamwe kujaribu kupata cho chote kutoka kwa Mungu bila kwanza kuwa sawa na Mungu. Mnaona? Na ndipo unaagizwa katika jambo hili kuwaita majirani zako, na mchungaji wako. Kama una kitu cho chote kilicho moyoni mwako dhidi ya mtu yeyote, nenda ukakitengeneze kwanza, kisha urudi. Kisha omba, fanya mkutano wa maombi nyumbani mwako, halafu ishikize lesu hii kwa pini kwenye nguo yako ya ndani, ndipo umwamini Mungu. Na kwenye vipindi hivyo vya masaa matatu, kila siku, kutakuwako na watu kote ulimwenguni wanaomba, mnyororo kote ulimwenguni.

6 Na sasa ni yako, bure kabisa, tuma tu. Na—na, sasa, hatutakuwa tukikuandikia kukutoza fedha au kukuambia miradi ya maendeleo tuliyo nayo. Tunakutaka uunge mkono miradi, lakini hatuna—hatuna wote kwako wewe kuunga mkono. Mnaona? Kwa hiyo wewe ... Si kwa madhumuni ya kupata anwani yako, ni kwa ajili ya kuratibisha tu na huduma ya Bwana ambayo tunajaribu kuendeleza.

Sasa hebu na tuinamishe vichwa vyetu. Na iwapo unasikiliza redio, weka lesu yako hapo, hebu weka tu mkono wako mwenyewe juu yake tunapomba.

7 Bwana Mwenye Neema, tunakuletea Wewe vijifurushi hivi vidogo, pengine baadhi yavyo vinaonekana kuwa labda vijifulana vidogo vya mtoto mchanga, au—au kijishati cha ndani, au pengine jozi ndogo ya viatu, au—au kitu fulani, lesu, inayopelekwa kwa mgonjwa na anayeteseka. Bwana, ni kulingana na Neno Lako kwamba tunafanya jambo hili. Kwa kuwa tunasoma, katika Kitabu cha Matendo, ya kwamba walichukua kutoka kwenye mwili wa mtumishi Wako, Paulo, lesu na nguo, kwa sababu waliamini ya kwamba Roho Wako alikuwa juu ya mtu huyo. Na pepo wachafu wakawatoka watu, na mateso na

magonjwa yakawaacha, kwa sababu waliamini. Na sasa tunatambua, Bwana, kwamba sisi sio Mtakatifu Paulo, bali tunajua kwamba Wewe bado ungali Yesu. Nasi tunaomba ya kwamba utaheshimu imani ya watu hawa.

8 Na ilisemwa wakati mmoja ya kwamba wakati Israeli, wakijaribu kumtii Mungu, walikuwa wamenaswa kwenye mtego, bahari mbele yao, milima pande zote mbili, na jeshi la Farao likija. Na mmoja amesema, ya kwamba "Mungu aliangalia kupitia kwenye ile Nguzo ya Moto, akiwa na macho yenye hasira, nayo bahari ikaogopa na kujifingirisha yenyewe, na kufanya njia kwa ajili ya Israeli kuvuka kwenda kwenye nchi ya ahadi."

Ee Bwana, angalia chini tena, wakati vifurushi hivi vimewekwa juu ya miili ya wagonjwa kwa ukumbusho wa Neno Lako lililo hai. Na jalia ugonjwa huu uogope, angalia kupitia Damu ya Mwanao, Yesu, ambaye alikufa kwa ajili ya upatanisho huu. Na jalia adui aogope na aondoke, ili kwamba watu hawa wapate kuingia katika ahadi, ya kwamba "Juu ya mambo yote," ya kwamba ni shauku Yako "kwamba tufanikiwe katika afya." Tujalie hilo, Baba, kwani tunalipeleka kwa hiyo—kwa hiyo nia moyoni mwetu. Na hilo ndilo kusudi letu. Tunalituma katika Jina la Yesu Kristo. Amina.

Asante, Ndugu Glover. Asante, bwana.

9 Sasa, usiku wa leo ukiwa ndio mwisho wa sehemu hii ya ufufuo, sijui kama itatangazwa au la, bali ningetaka kuwaambia (kama sivyo) kwa wasikilizaji wa redio, ya kwamba huu umekuwa mmoja wa mikutano mizuri sana. ambayo nimekuwa nayo kwa miaka mingi, mingi sana. Umekuwa ni mkutano thabiti, mzuri, wenye upendo sana, wa ushirikiano ambao nimekuwa nao kwa muda mrefu.

10 [Ndugu fulani anasema, "Tunatangazwa kwa redio hadi saa kumi na robo, ndugu. Nao wanakusikiliza, kote kusini mwa California, huko visiwani, na kwenye meli. Tunapata jumbe kutoka kwao. Na kwa hiyo mna kusanyiko kubwa, maelfu na makumi elfu." — Mh.] Asante, bwana. Hilo ni zuri sana. Ninafurahi kusikia hayo. Mungu awabariki nyote.

Na hakika sikuzote nimekuwa na shauku moyoni mwangu kwa Angelus Temple, kwa msimamo wake wa Injili kamili ya Yesu Kristo. Na, sasa, li—linaonekana la kibinafsi zaidi kwangu sasa. Inaonekana kama, baada ya kukutana na kila mmoja na kuona roho zao nzuri, yaelekea kama kwamba mimi ni mmoja wenu zaidi kuliko nilivyokuwa. Mungu akubariki, ndilo ombi langu. Na ... [Hadhira inashangilia — Mh.] Asanteni, sana.

11 Sasa, imetangazwa kwamba leo ningezungumza nanyi kwa kitambo juu ya: *Hadithi ya Maisha Yangu*. Hilo ni—ni jambo gumu kwangu. Hii itakuwa ni mara ya kwanza mimi nimejaribu kuiendea kwa miaka mingi. Nami singekuwa na wakati wa kueleza kwa kina, lakini sehemu yake tu. Na, humu ndani, nimefanya makosa mengi, nimefanya mambo mengi ambayo yalikuwa mabaya. Nami nitatamani, ya kwamba ninyi mlio kwenye redio na ninyi mliopo, kwamba msichukue makosa yangu kuwa mawe ya kujikwaa, bali mawe ya kukanyaga kuwaleta karibu na Bwana Yesu.

12 Halafu, usiku wa leo, kadi za maombi zitatolewa kwa ajili ya ibada ya uponyaji usiku wa leo. Sasa, tunapozungumza juu ya *ibada ya uponyaji*, haimaanishi ya kwamba tutamponya mtu fulani, "tutamwomba mtu fulani." Mungu hufanya uponyaji. Yeye amekuwa tu mwenye neema sana kwangu, kujibu maombi.

Nami nilikuwa nikizungumza na meneja wa mwinjilisti mashuhuri, hapa wakati fulani uliopita, na—na iliulizwa ni kwa nini mwinjilisti huyu hakuwaomba wagonjwa. Naye mwinjilisti akamwambia yule m—msimamizi wa mikutano yangu, akasema, "Kama ... Mwinjilisti huyu anaamini katika uponyaji wa Kiungu. Lakini kama angeanza kuwaomba wagonjwa, ingekatiza ibada yake kwa sababu amedhaminiwa na makanisa. Makanisa mengi, na mengi yao, hayaamini uponyaji wa Kiungu."

Kwa hiyo nina staha na heshima kwa mwinjilisti yule kwa sababu yeye ameshikilia mahali pake, wajibu wake. Yeye labda angeweza ... Nisingeweza kamwe kupachukua mahali pake, nami ninashuku kama angeweza kuchukua mahali pangu. Sisi sote tuna nafasi katika Ufalme wa Mungu. Sote tumeunganishwa pamoja. Karama mbalimbali, bali ni Roho yeye yule. Madhihirisho mbalimbali, nilimaanisha kusema, bali Roho yeye yule.

13 Na, sasa, usiku wa leo ibada zitaanza ... Nafikiri walisema uimbaji unaanza mnamo saa kumi na mbili u nusu. Na, sasa, kama uko nje kwenye redio, njoo usikilize jambo hili. Ni ... Utakuwa mzuri, ndivyo ilivyo sikuzote.

Na kisha nataka kusema kwamba kadi za maombi zitatolewa mara baada ya ibada hii, mara tu ibada hii inapokwisha, iwapo upo hapa nawe unataka kadi za maombi. Niliarifiwa ndani hapo muda mfupi tu uliopita, mwanangu au Bw. Mercer au Bw. Goad, watakuwa wakitoa kadi za maombi. Msiondoke kwenye viti vyenu. Mara tu ibada inapokwisha, hebu bakini kwenye viti vyenu ili wale vijana waweze kupita katika mstari na kutoa kadi za maombi haraka iwezekanavyo. Hilo litakuwa kwenye roshani au chumbani, po pote pale, vyumba vya chini au po pote ulipo, basi endeleeni kuketi na hao wavulana watajua

kwamba mnahitaji kadi za maombi. Na halafu usiku wa leo tutakuwa tukiwaombea wagonjwa. . Na iwapo Bwana hatabadili mawazo yangu, nataka kuhubiri juu ya somo usiku wa leo, *Kama Utatuonesha Baba, Itatutosha.*

14 Sasa nataka kusoma kwa ajili ya somo alasiri ya leo, kuanza tu Hadithi ya Maisha, inayopatikana katika Kitabu cha Waebrania, mlango wa 13, na hebu tuanzie hapa karibu ... Ningesema kuhusu kifungu cha 12.

Kwa ajili hii Yesu naye, ili awatakase watu kwa damu yake mwenyewe, aliteswa nje ya lango.

Basi na tutoke ... tumwendee nje ya kambi, tukichukua shutumu lake.

Maana hapa hatuna mji udumuo, bali twautafuta ule ujao.

Sasa hilo kwa namna fulani ni somo. Kwa maana, mnaona iwapo ni hadithi ya maisha, au jambo lote linalohusiana na mwanadamu, hatutukuzi jambo hilo, na hasa sana ma—maisha ya mtu yaliyopita, kama yamekuwa meusi kama yangu yalivyokuwa. Lakini nilifikiri, kama tukisoma Maandiko, Mungu angebariki Maandiko. Na wazo langu ni:

Kwamba hapa hatuna mji udumuo, bali twautafuta ule ujao.

15 Sasa, ninajua ya kwamba mnapenda sana Los Angeles. Mna haki ya kuupenda. Ni jiji maarufu, jiji zuri. Pamoja na mchanganyiko wake wa moshi na ukungu na kadhalika, hata hivyo ni jiji zuri, hali nzuri ya hewa. Lakini jiji hili haliwezi kudumu, halina budi kuwa na mwisho.

Nimesimama huko Rumi (ambako wafalme wakuu) na ile miji ambayo walidhani wangejenga idumuyo, na kuchimba chini futi ishirini kupata hata magofu yake.

Nimesimama ambapo Mafarao walikuwa na milki zao kuu, na ungechimbua chini katika ardhi kupata ambapo hao Mafarao wakuu walitawala.

Sisi sote hupenda kufikiria kuhusu jiji letu na mahali petu. Lakini, kumbukeni, haiwezi kudumu.

16 Nilipokuwa mvulana mdogo nilizoea kwenda kwenye mti mkubwa wa mepoo. Nchini mwangu tuna miti mingi migumu. Basi tulikuwa na huu mti wa mepoo, mepoo sukari, na tunaota "mepoo mgumu" na "mepoo laini." Huu mti mkubwa mno, ulikuwa ndio mti mzuri zaidi ya yote. Na wakati ningerudi kutoka mashambani, katika kazi ya nyasi za malisho na—na mavuno, nilipendelea kwenda kwenye mti huu mkubwa na—na kuketi chini yake na—na kuangalia juu. Nami ningeweza kuona matawi yake makubwa, yenye nguvu yakitikiswa na upepo, shina lake kubwa mno. Nami nikasema, "Unajua, ninaamini ya kwamba mti huu utakuwa hapa kwa mamia na mamia ya miaka." Si muda mrefu uliopita niliungalia ule mti wa kale, ni kisiki tu.

"Maana hapa hatuna mji udumuo." La, hakuna kitu hapa duniani ambacho unaweza kutazama kitakachodumu. Hakina budi kiwe na mwisho. Kila kitu ambacho hufa lazima kitoe nafasi kwa kisichopatikana na mauti. Kwa hiyo haidhuru barabara zetu kuu tunazijenga vizuri vipi, jinsi gani tunatengeneza majengo yetu, vyote havina budi kuharibika, kwa maana hapa hakuna kitu kinachoweza kudumu. Yasiyoonekana tu ndiyo yanayoendelea.

17 Nakumbuka nyumba ambayo tuliishi, ilikuwa nyumba ya kale ya magogo iliyokandikwa kwa matope. Mimi ... Pengine huenda wengi hawajawahi kuona nyumba iliyokandikwa kwa matope. Lakini yote ilikuwa imekandikwa kwa matope, na yale magogo makubwa mno yaliyokuwa katika hiyo nyumba ya kale, nilifikiri nyumba ile ingedumu kwa mamia ya miaka. Bali, mnajua, leo pale nyumba ile iliposimama pana mradi wa ujenzi wa nyumba. Ni tofauti sana. Kila kitu kinabadilika. Lakini ...

18 Nami nilikuwa nikimwona baba yangu, yeye alikuwa ni mtu mfupi, mnene, mwenye nguvu sana, naye alikuwa mmoja wa watu wenye nguvu kuliko wote niliowajua. Nilikutana na Bw. Coots, mtu ambaye alikuwa akifanya kazi naye katika magogo, alikuwa mkata magogo, basi yapata mwaka mmoja uliopita, na Bw. Coots ni rafiki yangu msiri, na ni shemasi katika kanisa la First Baptist, naye akasema, "Billy, huna budi kuwa mtu mwenye nguvu sana."

Nami nikasema, "La, sivyo, Bw. Coots."

Akasema, "Kama ulichukua maungo ya baba yako, ungekuwa hivyo." Kasema, "Nilimwona mtu huyo, mwenye uzito wa ratili mia na arobaini, akipakia gogo kwenye gari lake peke yake, ambalo lilikuwa na uzito wa ratili mia tisa." Alijua tu jinsi ya kufanya jambo hilo. Alikuwa na nguvu. Ningemwona akija mahali pa kunawia na kujitayarisha kwa chakula, mama anapomwita.

19 Nasi tulikuwa na mtofaa wa zamani nje katika uwanja, na halafu kulikuwa na mitatu au minne midogo upande wa nyuma. Na pale penye mti wa katikati kulikuwa na kioo cha kale cha kujiangalia, kimevunjika,

kioo, kikubwa. Na kilikuwa kimebandikwa ubavuni mwa ule mti kwa misumari iliyokunjwa. Ni kama ambayo baadhi yenu ninyi maseremala mnaosikiliza mngeita “misumari ya kutundikia koti.” Ilikuwa imeinama kushikilia kioo mahali pake. Na kulikuwa na kitana kikuukuu cha bati. Wangapi wamewahi kuona bati... kitana cha bati mtindo wa kale? Ninaweza tu kukiona.

Na halafu kulikuwa na benchi dogo la kunawia, ubao mdogo tu uliokuwa na mguu chini yake uliokaa upande, umepigiliwa kwenye ule mti. Bomba dogo kuukuu, la nusu salfa pale ambalo tulivutia maji, nasi tuliogea kwenye mti huu wa zamani. Naye Mama alikuwa akichukua magunia ya unga na kutengeneza taulo. Kuna mtu yeyote aliyewahi kutumia taulo ya gunia la unga? Vema, nina hakika ninajisikia nyumbani sasa. Na hizo taulo kubwa za kale zinazoparuzi! Na wakati alipotuogesa sisi watoto wadogo, ange... ilisikika kama alikuwa anasugua ngozi itoke kila wakati aliposugua. Nami ninakumbuka hilo gunia la kale la unga. Naye angechomoa baadhi ya nyuzi zake na kutengeneza vifundo vidogo, ili kulipamba kwa namna fulani.

20 Ni wangapi wamewahi kulala kwenye godoro la nyasi kavu? Vema, nita—nitasema! Wangapi wamewahi kujua mto wa makapi ulikuwa nini? Vema, Ndugu Glover, niko nyumbani sasa, hakika kabisa! Godoro la nyasi kavu, vema, haujapita muda mrefu sana tangu niache kulalia moja, na ilikuwa... Loo, ni—ni zuri la kulalia, baridi kidogo. Katika majira ya kipupwe huchukua kitanda cha zamani cha manyoya wakakilalia, unajua, halafu inabidi kutufunika kwa kipande cha turubai kwa sababu theluji iliingilia katika zile—zile—zile nyufa kwenye nyumba, mnajua, ambapo mbao kuukuu za kuzeekeka nyumba zingepishana, mnajua, na theluji ingepenya mle. Na, loo, ninaweza kukumbuka jambo hilo vizuri sana.

21 Na halafu Baba alipata kuwa na burashi ya kunyolea. Mimi ... Sasa hili litawachekesha. Ilitengenezwa kwa maganda ya mahindi, brashi ya kunyolea ya maganda ya mahindi. Angechukua sabuni ya kale ya mama ya magadi ambayo alitengeneza, akaitayarisha na akajipaka usoni kwa brashi hii ya maganda ya mahindi, na kuzinyoa kwa wembe mkubwa wa kale ulionyooka. Na Jumapili angechukua vi—vipande vya karatasi, akavibandika kuuzunguka ukosi wake, walivaa ukosi wa karatasi ngumu na kuizungushia kwenye ukosi namna hii kuhifadhi po—po—povu lisiguse ukosi wa shati lake. Mmewahi kuona hilo likifanywa? Mbona, jamani, jamani!

22 Ninakumbuka chemchemi ndogo chini huko, tulikozoea kwenda kuchota maji ya kunywa, na kuchota maji yetu kwa kata ya kale ya kibuyu. Wangapi wamewahi kuona kata ya kibuyu? Vema, ni wangapi wenu wanaotoka Kentucky, hata hivyo? Naam, vema, hebu angalieni tu hapa Wakentucky. Vema, jamani, nina—niko moja kwa moja kwenye ... Nilifikiria wote walio hapa ni Okies na Arkies, bali inaonekana kama Kentucky inaingia. Naam, walivumbua mafuta huko Kentucky miezi michache iliyopita, mwajua, kwa hiyo pengine hao ni baadhi yao wanaokuja huku.

23 Na halafu ninakumbuka wakati Baba alipokuwa anakuja na kunawa kwa ajili ya chakula, angekunja mikono ya shati lake, na hiyo mikono mifupi na minene. Na alipokunja mikono yake apate kunawa, akajitupia maji usoni mwake, hiyo misuli ilijaa tu kwenye mikono yake midogo. Nami nikasema, “Unajua, baba yangu ataishi miaka mia moja na hamsini.” Alikuwa na nguvu sana! Lakini alikufa akiwa na umri wa miaka hamsini na miwili. Mnaona? “Hapa hatuna mji udumuo.” Hiyo ni kweli. Hatuwezi kuendelea.

24 Sasa hebu na tusafiri kidogo, sisi sote. Kila mmoja wenu hapa ana hadithi ya maisha yake, kama niliyo nayo mimi, na ni vizuri kutembea katika barabara ya kumbukumbu mara kwa mara. Hivi hamwoni hivyo? Kurudi tu, na hebu sote turudi kwa muda, nyuma kwenye maisha sawa na hayo kama watoto wadogo.

Na sasa sehemu ya kwanza ya hadithi ya maisha. Nitaigusia kidogo tu, maana iko katika kile kitabu na wengi wenu mna kitabu hicho.

25 Nilizaliwa katika kibanda kidogo mlimani, juu huko kwenye milima ya Kentucky. Walikuwa na chumba kimoja ambamo tuliishi, hapakuwa na zulia sakafuni, hakuna hata mbao sakafuni, ilikuwa tu udongo mtupu. Na gogo, sehemu ya juu ya gogo iliyokatwa yenye miguu mitatu, hiyo ndiyo iliyokuwa meza yetu. Na hao watoto wote Wabranham wangekusanyika kuizunguka, na huko nje mbele ya kile kibanda kidogo cha kale, na kugaagaa kabisa, ilionekana kama kwamba kundi la komba wamekuwa wakigaagaa kule nje kwenye vumbi, mwajua, wale ndugu wadogo wote. Tulikuwa tisa, na msichana mmoja mdogo, naye kweli alikuwa na wakati mgumu miongoni mwa kundi hilo la wavulana. Hatuna budi kumheshimu bado leo kutokana na mambo tuliyofanya katika siku hizo. Hangeweza kufuatana nasi mahali po pote, tungelimfukuza arudi, alikuwa msichana. Kwa hiyo asingeweza kuyastahimili hayo, mnajua. Kwa hiyo tulikuwa ... Na wote ...

26 Kumbuka kwamba huko nyuma ya meza tulikuwa na viti viwili tu, na vilitengenezwa kutokana na gome la tawi. Ni vitawi vidogo vya mti mgumu vikiunganishwa pamoja, na sehemu ya chini imesukwa pamoja kwa gome la mti huo. Yupo aliyewahi kuona kiti cha gome la mti mgumu? Naam. Nami ninaweza kumsikia Mama bado. Loo, baadaye tulipofikia mahali ambapo angeweza kupata sakafu ya mbao, akiwa na wale watoto wachanga pajani mwake namna hii, na akibembea kile kiti cha kale huku kinalia bankti, bankti, kishindo sakafuni. Na ninakumbuka ili kuwazuia watoto wasitoke nje ya mlango, wakati yeye

anafua au kitu fulani, angelaza kiti chini na kukigeuza kwa namna fulani kikingame mlangoni, ili kuwazuia watoto wasitoke nje wakati ilipombidi kwenda kwenye chemchemi kuchota maji, na kadhalika.

Naye Mama alikuwa na umri wa miaka kumi na mitano nilipozaliwa, Baba alikuwa na umri wa miaka kumi na minane. Nami nilikuwa wa kwanza kati ya hao watoto tisa. Nao waliniambia ya kwamba asubuhi niliyozaliwa ...

27 Naam, tulikuwa fukara sana, maskini wa maskini. Nasi hatukuwa hata na dirisha katika kijumba hiki kidogo. Kilikuwa na kitu kama mlango mdogo wa mbao ambao mnafungua. Nina shaka kama umewahi kuona kitu kama hicho. Mlango mdogo wa mbao ambao ulifunguka badala ya dirisha, unauacha wazi mchana na kuufunga usiku. Hatukuweza kuwasha taa za umeme au hata za mafuta ya taa siku hizo, tulikuwa na inayoitwa "taa ya shahamu." Sasa, sijui kama uliwahi kujua taa ya shahamu ilikuwa nini. Vema, ninyi mna... Na uliwahi kununua...kuwasha fundo la msonabari? Maana unachukua tu fundo la msonabari na kuliwasha na kuliweka juu ya kifuniko, litawaka. Na hiyo ni...lilifuka moshi kidogo, lakini hawakuwa na fanicha, hata hivyo, ya kutia masizi. Kwa hiyo kili...kibanda kilipata masizi. Ulitoka vizuri sababu kulikuwa na paa la kutosha juu kule kwa huo kutokea. Kwa hiyo ni ...

28 Basi nilizaliwa Aprili ta—tarehe 6, 1909. Bila shaka, mnajua, hilo lanifanya niwe na umri uliozidi kidogo miaka ishirini na mitano sasa. Na kwa hiyo, asubuhi niliyozaliwa, Mama alisema ya kwamba walifungua dirisha. Sasa, hatukuwa na madaktari, kulikuwako na mkunga. Ninii tu ... Na huyo mkunga alikuwa bibi yangu. Na kwa hiyo nilipozaliwa na kulia kwangu kwa kwanza, na—na Mama alitaka kumwona mtoto wake. Na—na yeye alikuwa mwenyewe ni mtoto tu. Na walipofungua hilo dirisha dogo, wakati wa mapambazuko, yapata saa kumi na moja. Na ninii ... Alikuweko maskini robin ametua kando ya kichaka kidogo. Kama ninyi nyote mlivyokwisha kuona picha yake katika—katika kitabu changu cha hadithi ya maisha yangu. Maskini robin alikuwa ametua pale akiimba kwa bidii sana.

29 Nimewapenda robin sikuzote. Sasa, ninyi wavulana mnaosikiliza redio huko nje, msiwaue hao ndege wangu. Mnaona, wao ni—wao ni—wao ni... Wao ni ndege wangu. Je! Ulipata kusikia hadithi ya robini, jinsi alivyopata kifua chake chekundu? Nitasimama hapa kwa muda kidogo. Jinsi alivyopata kifua chake chekundu ... Kulikuwa na Mfalme wa wafalme anakufa siku moja Msalabani, na Yeye alikuwa anateseka na hakuna mtu aliyekuja Kwake. Hakuwa na mtu wa kumsaidia. Na palitokea ndege mdogo mwenye rangi ya kahawia aliyetaka kuiongoa hiyo misumari Msalabani, basi akaendelea kuruka pale Msalabani na kuvuta misumari ile. Alikuwa mdogo mno asingeweza kuing'oa, basi kifua chake kidogo kikalowa damu. Na tangu wakati huo kifua chake kimekuwa chekundu. Msimuue, enyi wavulana. Mwacheni.

Alikuwa ameketi kando ya dirisha, akiimba kama waimbavyo robin. Basi—basi Baba alifungua dirisha. Na walipolifungua lile dirisha la mlango mdogo, Nuru ile ambayo mnaiona kwenye picha ikaja inazunguka dirishani, asema mamangu, na ikaning'inia juu ya kitanda. Bibi hakujua la kusema.

30 Sasa, sisi ni ... haikuwa familia ya kidini. Watu wangu ni Wakatoliki. Mimi ni Mwairishi pande zote mbili. Baba yangu ni Muairishi halisi, Branham. Mama yangu ni Mharvey; ni kwamba tu, baba yake alimuoia Mhindi wa Cherokee, kwa hiyo hilo lilivunja huo ukoo mdogo au damu ya Kiairishi. Na Baba na Mama hawakwenda kanisani, na walioana nje ya kanisa na hawakuwa na dini hata kidogo. Na nyuma huko kwenye milima hakukuwa hata na kanisa la Kikatoliki. Kwa hiyo walikuja wakati wa masetla wa kwanza, Wabranham wawili wakaja, na kutoka kwa hao kukatokea kizazi kizima cha Wabranham; ndio ukoo wa familia.

31 Na ndipo akafungua ... Walipofungua dirisha hili na Nuru hii ikaning'inia mle ndani, hawakujua la kufanya. Baba aliishajinunulia (Mama alisema) ovaroli mpya kwa ajili ya tukio hili. Alikuwa amesimama na... huku ametia mikono yake kwenye sehemu ya mbele ya hiyo ovaroli kuukuu, kama vile wakata miti na wakata magogo walivyozoea katika siku zile. Na iliwaogopesha.

32 Naam, baada ya kufikia labda umri wa siku kumi, au kitu kama hicho, walinipeleka kwenye kanisa dogo la Kibatisti linaloitwa "Opossum Kingdom," kanisa la Kibatisti la Opossum Kingdom. Hilo ni jina kwelikweli. Kulikuwa na mhubiri wa kuzunguka huku na huko, mhubiri wa Kibatisti wa mtindo wa kale alizuru mahali hapo mara moja kila miezi miwili. Kwenye ... Watu wangefanya ibada ndogo pamoja, wangeenda waimbe nyimbo, bali walikuwa na mahubiri mara kwa mara toka kwa mhubiri yule wa mzunguko. Walimlipa kila mwaka kwa gunia la maboga na vitu vichache kama hivyo, unajua, ambavyo watu walilima wapate kumpa yeye. Na huyo mhubiri mzee akaja, na hapo alinifanyia maombi kama mvulana mdogo. Hiyo ilikuwa ndiyo safari yangu ya kwanza kanisani.

33 Kwenye mwaka wa kama...kitu kama umri unaozidi kidogo miaka miwili, ono la kwanza lilitokea.

Naam, walikuwa wamelitangaza sehemu zote za milimani kule kwamba "Nuru hii iliingia." Kwa hiyo walijaribu kuliwazia. Baadhi yao walisema lazima ilikuwa nuru ya jua ikirudisha nuru toka kwenye kioo humo nyumbani. Lakini hakukuwa na kioo mle ndani. Na jua halikuwa limechomoza, kwa hiyo ilikuwa mapema mno, saa kumi na moja. Hivyo basi, loo, wakaipuuza Hiyo. Nami nilipokuwa na kama...nadhani kuwa na umri wa karibu miaka mitatu...

34 Sasa, sina budi kuwa mwaminifu. Kuna mambo hapa ambayo sitaki kuyasema, nami laiti ningeweza kuyaruka na isinibidi kuyasema. Bali hata hivyo, kusema kweli, yakubidi useme ukweli kama ni juu yako mwenyewe au watu wako. Uwe mwaminifu kuhusu jambo hilo, ndipo sikuzote ni jambo lile lile.

Baba yangu alikuwa mbali na kuwa mtu wa dini. Yeye alikuwa mvulana halisi wa mlimani ambaye alikunywa pombe daima, wakati wote. Naye aliingia katika matatizo ya kupigana, na kulikuwa na watu wawili au watatu karibu wauawe wakati wao walipopigana, wakitupiana risasi, na kukatana visu, kwenye namna fulani ya tafrija huko milimani. Na Baba alikuwa mmoja wa viongozi wa kundi la mapigano haya, kwa sababu kulikuwa na rafiki yake aliyeumizwa, na amempiga mtu fulani kwa kiti. Na alikuwa ... Huyo mtu alichomoa kisu na alikuwa anataka kumchoma rafiki ya Baba kwa kisu sakafuni, kumchoma moyoni, basi Baba akashiriki. Na kwa kweli vilikuwa vita vikali sana, kwa sababu wao, kutoka mbali chini huko hadi Burkesville, umbali wa maili nyingi, walimtuma liwali kumfuatilia Baba, juu ya farasi.

35 Kwa hiyo mtu huyo alikuwa amelala akiwa nusura kufa. Yawezekana baadhi ya watu wake wanasikiliza. Nitataja jina lake, jina lake aliitwa Will Yarbrough. Labda wao ... Nadhani wao wako California, baadhi ya wanawe. Lakini alikuwa mjeuri, mtu mnene mwenye nguvu, alimua mwanawe kwa ufito wa ua. Kwa hiyo yeye—yeye alikuwa mtu mwenye nguvu sana na mwovu. Na kwa hiyo palikuwa na vita vikali vya visu kati yake na Baba. Na baba yangu karibu amue yule mtu, kwa hiyo ilimbidi akimbie aondoke Kentucky avuke mto hadi Indiana.

36 Basi yeye alikuwa na kaka ambaye aliishi, wakati huo, huko Louisville, Kentucky, alikuwa kaimu msimamizi wa Kiwanda cha Mbao cha Mosaic huko Kentucky, huko Louisville. Na kwa hiyo Baba akaja kumkuta kaka yake. Baba alikuwa kitinda mimba katika wavulana, kwa watoto kumi na saba. Na kwa hiyo alikuja kumtafuta kaka yake, na wakati ambapo alikuwa ameondoka kwa karibu mwaka mmoja. Hangeweza kurudi, kwa sababu sheria ilikuwa inamtafuta. Na ndipo tulipopata habari kutoka kwake kwa barua, iliyotiwa sahihi kwa jina jingine, lakini kwamba yeye alikuwa amemwambia mama jinsi angewasiliana naye.

37 Kisha ninakumbuka siku moja chemchemi ile (kibanda hiki kidogo) ilikuwa tu nyuma ya nyumba. Na—na katika wakati huo baada ya ... Kuna tisa...tofauti ya miezi kumi na mmoja kati yangu na ndugu yangu anayenifuata, na yeye bado alikuwa anatambaa. Basi nilikuwa na jiwe kubwa mkononi mwangu, na nilikuwa nikijaribu kumwonyesha yeye jinsi ambavyo ningeweza kulitupa jiwe hili kwenye matope, mahali ambapo chemchemi ilibubujika toka ardhini na kuifanya ardhi iwe topetope. Ndipo nikasikia ndege, na alikuwa akiimba juu ya mti. Basi niliangalia juu kwenye mti ule na yule ndege akaruka akaenda zake, na, wakati alipoondoka, Sauti ilinena nami.

Sasa, najua mnafikiri nisingeweza kufikiri na kukumbuka jambo hilo. Bali Bwana Mungu Ambaye ndiye Hakimu, wa mbingu na nchi na yote yaliyomo, anajua ninasema kweli.

38 Ndege yule, aliporuka kwenda zake, Sauti ilikuja kutoka mahali yule ndege alipokuwa juu ya mti, kama upepo ulioshikwa katika kijiti, na Hiyo ikasema, "Utaishi karibu ya mji unaoitwa New Albany." Nami nimeishi, tangu nilipokuwa na umri wa miaka mitatu mpaka wakati huu, katika maili tatu kutoka New Albany, Indiana.

Niliingia ndani na kumwambia mama yangu kuhusu jambo hilo. Vema, alidhani nilikuwa nikiota tu ama kitu fulani.

Na baadaye tulihamia Indiana na baba akaenda kufanya kazi kwa mtu mmoja, Bw. Wathen, mtu tajiri. Ni mwenye Kiwanda cha Wathen cha kutengenezea mvinyo. Basi alikuwa na hisa nyingi sana; yeye ni milionea kwelikweli, na Louisville Colonels, na—na gofu, na kadhalika. Na kisha tuliishi karibu na mahali pale. Na Babangu akiwa maskini, hata hivyo hangeweza kuacha ulevi wake, kwa hiyo aka—akaanza kutengeneza chang'aa kwa—kwa chombo cha kutengenezea chang'aa.

Ndipo tukio hili likanilemea sana kwa sababu nilikuwa ndiye mkubwa wa watoto wote. Ilinibidi nije niteke maji kupeleka kwenye chombo hiki cha kutengenezea chang'aa, kupoza mifereji ile wakati walipokuwa wanatengeneza chang'aa. Basi akawa anaiuza, na halafu akapata vyombo viwili au vitatu vya chang'aa. Sasa, hiyo ndiyo sehemu nisyopenda kusimulia, bali ni kweli.

39 Ndipo nakumbuka siku moja, toka kwenye ghala la nafaka, nikipanda kwenda nyumbani, nikilia. Kwa sababu nje huko nyuma ya mahali hapo kulikuwa na kidimbwi, ninii ...ambapo walitumia kukatia barafu. Wengi wenu mnakumbuka wakati walipozoea kukatakata barafu na kuiweka kwenye unga wa mbao. Naam, hiyo ndiyo namna Bwana Wathen alivyohifadhi barafu nje huko kijijini. Na Baba alikuwa de—dereva wake, dereva wa binafsi. Na wakati hili...dimbwi hili lilikuwa linajaa samaki wakati wangeenda kukatakata barafu na kuileta na kuiweka kwenye unga wa mbao, basi wakati barafu ile ilipoyeyuka wakati wa msimu wa kiangazi wakati ilipokuwa inazama, nadhani ilikuwa safi kidogo, zaidi kama ziwa la barafu, nao waliweza kuitumia, sio kwa kunywa, bali kwa kuyahifadhi maji baridi, waliweka kandokando ya ndoo zao na maziwa yao na kadhalika.

40 Basi siku moja nilipokuwa nikibeba maji toka nyuma nje kwenye bomba hili, ambalo lilikuwa umbali wa kama jengo moja la mji. Nilikuwa namlilia kwa nguvu mtu ambaye hangenisikiliza, kwa sababu nilikuwa nimetoka shuleni na wavulana wote walikuwa wamekwisha kwenda bwawani, kuvua samaki. Nilipenda tu kuvua samaki. Na kwa hiyo wote walienda kuvua isipokuwa mimi, na ilinibidi kubeba maji ya chombo hiki cha chang'aa. Bila shaka, jamani, lilibidi lifanywe kisirisiri, ilikuwa imepigwa marufuku. Nami ... Lilinilemea sana. Nami nakumbuka nikija pale huku kidole gumba cha mguu wangu kimepondwa, na nimefunga gunzi chini ya kidole gumba changu kukikinga na vumbi. Uliwahi kufanya hivyo? Kuweka tu gunzi la mahindi chini ya kidole gumba chako namna hii na kulifunga kwa kamba. Linakishikilia kidole gumba chako juu kama vile kichwa cha kasa, mnajua, kikitokeza juu. Ungeweza kunifuatilia kila mahali nilipoenda, nikiwa na gunzi hili la mahindi chini ya kidole gumba; mahali nilipokanyaga, mnajua. Sikuwa na viatu vya kuvaa. Kwa hiyo hatukuvaa viatu, wakati mwingine nusu ya majira ya baridi kali. Kama tulivaa, sisi...ilikuwa tu ambavyo tuliweza kuokota, mtu fulani angetupa sisi. Na nguo ambazo mtu fulani, ambazo tungezipata kwa hisani.

41 Nami nikasimama chini ya mti huu, na nilikuwa nimekaa pale nikilia sana (ilikuwa Septemba) kwa sababu nilitaka kwenda kuvua, ilinibidi kujaza maji mapipa kadha kwa ndoo za sukari guru, kama urefu huu tu, nusu galoni, sababu nilikuwa mvulana mdogo tu wa kama umri wa miaka saba. Nami ningezimwaga kwenye pipa kubwa halafu nirudi na kuchota ndoo nyingine mbili na kurudi, kuyasukumiza kwenye bomba. Hayo ndiyo maji tuliyokuwa nayo. Nao walikuwa watengeneze chang'aa ya mahindi usiku ule, watu hawa pamoja na Babangu, kule nyumbani.

42 Basi nilikuwa nikilia, mara nikasikia kitu kikifanya uvumi kama wa upepo wa kisulisuli, kitu kama hiki (sasa, natumaini si mkubwa mno), ukivuma, "Whooooosssh, whoooooosssh," uvumi tu kama huo. Naam, kulikuwa kimya sana, nami nikaangalia pande zote. Wajua, upepo mdogo wa kisulisuli, naamini mnaita vimbunga vidogo? Kwenye majira ya kupukutisha majani vinabeba kwenye shamba la mahindi, mnajua, majani na kadhalika, katika msimu wa masika kule, majani yanapoanza tu kugeuka. Nami nilikuwa chini ya mti mkubwa mweupe wa mtakawa, nikisimama karibu kati ya ghala na ile—ile nyumba. Nami nikasikia kelele hiyo. Ndipo nikaangalia kote, kulikuwa kimya tu kama ilivyo katika chumba hiki. Hakuna jani linalovuma mahali po pote, wala cho chote kile. Nami nikawaza, "Hiyo kelele inatoka wapi?" Vema, nikawaza, "Lazima uwe mbali na hapa." Mvulana mdogo tu. Ukazidi kuwa mkubwa.

43 Nikachukua ndoo zangu na nikalia mara nyingi zaidi kisha nikaanza kutembea nikipanda kwenye kile kijia, nilikuwa ninapumzika. Ndipo nikatembea futi chache tu toka pale, kutoka chini ya matawi ya mti huu mkubwa, na, loo, jamani, ulitoa sauti ya upepo wa kisulisuli. Nami nikageuka kuangalia, na yapata urefu wa nusu ya mti ule kulikuwepo na upepo mwingine wa kisulisuli, umenaswa kwenye ule mti ukizungukazunguka, ukitikisa majani yale. Naam, sikuwazia cho chote kigeni kuhusu hilo kwa sababu ni katika wakati ule wa mwaka, na masika, mbona, hizo pepo za kisulisuli huja. Ndogo ... Tunaziita "pepo za kisulisuli." Na hizo—na hizo huzoa mavumbi. Mmeziona kwenye jangwa namna hiyo. Jambo lile lile. Kwa hiyo niliangalia, lakini haukuondoka. Kwa kawaida huwa ni mngurumo kwa muda mfupi sana, kisha huondoka, lakini ulikwisha kuwepo hapo dakika mbili au zaidi.

44 Naam, nikaanza kutembea nikipanda kwenye kile kijia tena. Ndipo niligeuka kutazama hili tena. Na Huo ulipofanya hivyo, Sauti ya kibinadamu inayosikika tu wazi kama yangu inavyosikika, ilisema, "Usinywe pombe kamwe, kuvuta sigara au kuuchafua mwili wako kwa namna yo yote. Kuna kazi utakayofanya utakapokuwa mtu mzima." Mbona, ilinitisha nusura nife! Ungeweza kuwazia jinsi mtoto mdogo alivyojisikia. Niliangusha ndoo zile, nikatimua mbio kuelekea nyumbani upesi nilivyoweza, nikipiga mayowe kwa upeo wa sauti yangu.

45 Na kulikuwa na vichwashaba nchini, nyoka, nao wana sumu sana. Mama alifikiria, ati nimemkanyaga huyo kichwashaba nilipokuwa nikija kando ya bustani, ndipo akakimbia akija kunichukua. Basi nikaruka juu hata kwenye mikono yake, huku ninapiga mayowe, nikimkumbatia na kumbusu. Naye akasema, "Kuna nini, umeumwa na nyoka?" Akaniangalia kila mahali.

Nikasema, "La, Mama! Kuna mtu kwenye mti ule kule chini."

Naye akasema, "Loo, Billy, Billy! Njoo?" Kisha akasema, "Ulisimama ukasinzia?"

Nikasema, "La, mama! Kuna mtu kwenye mti huo, Naye aliniambia nisinywe pombe wala nisivute sigara."

46 Kunywa wiski na—na kadhalika." Nami nilikuwa ninabeba maji kupeleka kwenye chombo cha kutengenezea chang'aa, wakati uo huo. Naye akasema, "Usinywe pombe kamwe au kujichafua mwili kwa namna yo yote." Hiyo ni kusema uchafu, mnajua, na utoto wangu...ujana na wanawake. Na nijuavyo mimi, sijawahi hata wakati mmoja kuwa na hatia ya jambo hilo. Bwana alinisaidia kwa mambo hayo, na nikiendelea mbele mtafahamu. Kwa hiyo basi, "Usinywe pombe wala usivute sigara, au usiuchafue mwili wako, kwani kuna kazi utakayofanya utakapokuwa mkubwa zaidi."

Vema, nilimwambia Mama jambo hilo, na—naye akanicheka tu. Nami nilikuwa na kiwewe sana.

Akamwita daktari, na daktari akasema, "Vema, ana wasiwasi tu, hivyo tu." Kwa hiyo akaniweka kitandani. Nami kamwe, tangu siku hiyo hadi hii, sijapita kwenye mti huo tena. Niliogopa. Ningeshuka kupitia upande wa pili wa ile bustani, kwa sababu niliwaza kulikuwa na mtu juu kwenye ule mti na Yeye alikuwa anazungumza nami, Sauti nzito mno ambayo ilinena.

47 Na halafu wakati fulani yapata mwezi mmoja baadaye, nilikuwa ninacheza gololi kule nje na ndugu zangu wadogo, mbele ya nyumba. Mara nikahisi hali ya ajabu ikinijia. Basi nikatulua na kuketi chini kando ya mti. Nasi tulikuwa huko juu ya ukingo toka kwenye Mto Ohio. Nikaangalia chini kuelekea Jeffersonville, na nikaona daraja likiinuka na kuingama huo, mto huo, kuvuka mto huo. Kisha nikaona watu kumi na sita (niliwahesabu) ambao walianguka kutoka huko na kupoteza maisha yao kwenye daraja lile. Nilikimbia ndani haraka sana na kumwambia mama, naye akadhani nililala usingizi. Bali jambo hilo waliliweka moyoni, na miaka ishirini na miwili tangu wakati huo Daraja la Manispaa sasa (ambalo wengi wenu mnalivuka mnapoenda ng'ambo ya pili) lilikatiza mto ule mahali pale pale, na watu kumi na sita walipoteza maisha yao wakijenga daraja lile kukatiza ule mto.

Haijashindwa kamwe kuwa kweli kabisa. Kama mnavyoiona Hiyo hapa kwenye jumba la mikutano, ndivyo imekuwa sikuzote.

48 Sasa, walidhani nilikuwa na wasiwasi tu. Ambapo, mimi ni mtu mwenye wasiwasi, hiyo ni kweli. Na, kama ukipata kuona, watu walio—wanaopenda kuwa wa kiroho wana wasiwasi.

Waangalie washairi na manabii. Hebu mwangalie William Cowper ambaye aliandika wimbo ule maarufu, "Damu imebubujika, ni ya Imanueli." Je, ulipata ... Unajua wimbo huo. Nilisimama karibu na kaburi lake si muda mrefu uliopita. Ndugu Julius, ninaamini, sijui, la...ndiyo, hilo ni kweli, alikuwa pamoja nasi kule kwenye kaburi lake. Na—na hapo, baada ya yeye kuandika wimbo huo, uvuvio ulikuwa umemtoka, akajaribu kuutafuta ule—ule mto ajiue. Mnaona, ile roho ilikwishamwacha. Na watu kama washairi na waandishi na...au sivyo...ninamaanisha manabii.

49 Mwangalie Eliya, wakati aliposimama mlimani na kuita moto kutoka mbinguni na kuita mvua kutoka mbinguni. Ndipo wakati Roho alipomwacha, alikimbia kwa tishio la mwanamke. Na Mungu alimkuta amejificha pangoni, siku arobaini baadaye.

Mwangalie Yona, ana uvuvio wa kutosha wakati Bwana alipompaka mafuta kuhubiri kule Ninawi, mpaka m—mji wenye ukubwa wa Saint Louis ukatubu kwa nguo za magunia. Halafu basi wakati Roho alipomwacha, ni kitu gani kilichompata? Tunamwona huko juu mlimani baada ya Roho kuondoka kwake, akimwomba Mungu achukue uhai wake. Na, mnaona, ni uvuvio. Na mambo haya yanapotukia lina—linatenda jambo fulani kwako.

50 Halafu ninakumbuka nilipoendelea kukua. Sina budi kuwa kijana. (Nitaharakisha kufanya hivyo katika muda mfupi ujao.) Nilipofika kuwa kijana nilikuwa na mawazo kama vijana wote wa kiume. Mimi...nikienda shuleni, niliwaona hao wasichana wadogo. Mnajua, nilikuwa na haya sana, na mnajua. Basi ha—hatimaye nikajipatia rafiki mdogo msichana. Na kama wavulana wote wadogo, kama umri wa miaka kumi na mitano, nadhani. Na—na kwa hiyo, loo, alikuwa mrembo. Jamani, alikuwa na macho kama ya hua, na alikuwa na meno kama lulu, na shingo kama ya korongo na a—alikuwa mrembo kweli.

51 Na mvulana mwingine mdogo, yeye...tulikuwa marafiki, kwa hiyo alichukua Ford aina ya T ya zamani ya baba yake, tukapeana miadi na wasichana wetu. Na tulikuwa tunaenda kuwachukua kwenda matembezini, kwa gari. Tulikuwa na za kutosha kununua galoni mbili za petroli. Ilitubidi kuwekea jeki gurudumu la nyuma tupate kupiga hendeli liondoke. Sijui kama mwaweza kukumbuka hilo au la, mnajua, kupiga hendeli. Lakini sisi—tulikuwa tukiendelea vizuri sana.

Na kwa hiyo nilikuwa na hela chache mfukoni mwangu, na tulisimama kituo fulani kidogo tukanunua... ungeweza kupata sambusa ya nguruwe kwa hela moja. Na kwa hiyo, loo, nilikuwa tajiri, ningeweza kununua nne! Mnaona? Na baada ya kula zile sambusa na kunywa koka kola. Nikaanza kurudisha chupa. Basi nikashangaa, nilipotoka kule, (wanawake walikuwa wameanza tu kupungukiwa na neema wakati ule, au kuacha utu uke) maskini hua wangu alikuwa anavuta sigara.

52 Naam, sikuzote nilikuwa na wazo langu kuhusu mwanamke ambaye angevuta sigara, na sijabadilisha kipengele kimoja tangu wakati ule. Hiyo ni kweli. Ni kitu duni sana awezacho kutenda. Na hilo ni kweli kabisa. Nami ni—nilifikiri nilininii ... Sasa, kampuni ya sigara ingeweza kunichukulia hatua kwa jambo hili, bali, ninawaambia, huo ni mkogo wa Ibilisi. Ndiyo muuaji mkubwa sana na mhalifu taifa hili liliye naye. Afadhali mwanangu awe mlevi kuliko awe mvuta sigara. Hiyo ni kweli. Afadhali nimwone mke wangu amelala sakafuni, amelewa, kuliko kumwona akiwa na sigara. Hivyo ndivyo ...

53 Sasa, huyu Roho wa Mungu ambaye yuko pamoja nami, kama Huyo ni Roho wa Mungu (kwa kuwa huenda mkatilia shaka), ninyi mnaovuta sigara mna nafasi ndogo mtakapofika kule, sababu hiyo tu...kila wakati. Mnaona kwenye jukwaa, jinsi Yeye anavyoilaani. Ni jambo la kutisha sana. Achaneni na kitu hicho. Mabibi, iwapo mmekuwa na hatia katika kitu hicho, tafadhali, katika Jina la Kristo, kiachenii!

Kinawaangamiza. Kitakuua. Kitaninii ... Ni—ni kansa chungu nzima.

Madaktari wanajaribu kukutahadharisha. Na halafu jinsi wanavyoweza kukuuzia takataka hiyo! Kama ungeenda kwenye duka la dawa na kusema, "Nunua... Ninataka kununua kansa ya senti hamsini." Mbona, wangukuja kuwafunga. Lakini unaponunua sigara zenye thamani ya senti hamsini, unanunua kitu kile kile. Madaktari wanasema hivyo. Loo, taifa hili lenye kichaa cha fedha. Ni mbaya sana. Ni mwuaji. Imethibitishwa.

54 Naam, nilipomwona msichana yule mrembo akijifanya mjanja, sigara hii mkononi mwake, hilo nusura liniue, maana kwa kweli nilifikiria nilimpenda. Nami nikawaza, "Vema ..."

Sasa, mimi huitwa "mchukia-wanawake," mnajua hilo, kwa sababu sikuzote kwa namna fulani nawapinga wanawake, bali mimi si dhidi yenu ninyi akina Dada. Mimi ninapinga tu jinsi wanawake wa kisasa wanavyotenda. Hiyo ni kweli. Wanawake wazuri wanapaswa kusifiwa.

55 Lakini naweza kukumbuka wakati chombo cha baba cha kutengeneza chang'aa juu kule kilipokuwa kinafanya kazi, ilinibidi kuweco nje huko na maji na kadhalika, kuona bibi wadogo ambao hawakuwa na zaidi ya umri wa miaka kumi na saba, kumi na minane, juu kule na wanaume wa umri wangu wa sasa, wamelewa. Na iliwabidi kuwalevusha kwa kuwapa kahawa nyeusi, wapate kurudi nyumbani kuwapikia chakula cha jioni waume zao. Loo, kitu kama hicho, nilisema, "Mimi ..." Nilitoa tamshi hili wakati huo, "Hawastahili risasi safi na nzuri ya kuwaua." Hiyo ni kweli. Nami niliwachukia wanawake. Hiyo ni kweli. Nami yanibidi nichunguze kila hatua sasa, kujiepusha na kuwaza jambo lile lile.

56 Kwa hiyo, bali sasa, mwanamke mzuri ni lulu katika taji ya mwanamume. Anapaswa kuheshimiwa. Yeye ... Mama yangu ni mwanamke, mke wangu vile vile, nao ni wazuri sana. Nami nina maelfu ya Dada Wakristo ambao ninawaheshimu sana. Bali kama—kama wanaweza kuheshimu kile Mungu alichowafanya, umama na malkia wa kweli, hilo ni sawa. Yeye ni moja ya mambo mazuri sana ambayo Mungu angeweza kumpa mwanamume, ilikuwa ni mke. Kando ya wokovu, mwanamke ndicho kitu kizuri zaidi ya vyote kama yeye ni mke mzuri. Bali iwapo yeye sivyo alivyo, Sulemani alisema, "Mwanamke mwema ni lulu katika taji ya mwanamume, bali aliye m—mkaidi au asiyefaa ni maji damuni mwake." Na hiyo ni kweli, ndilo jambo baya sana linaloweza kutukia. Kwa hiyo mwanamke mzuri ... Kama una mke mwema, ndugu, yakupasa kumheshimu sana. Hiyo ni kweli, unapaswa kufanya hivyo. Mwanamke halisi! Pia, enyi watoto, kama mna mama halisi ambaye hukaa nyumbani akijitahidi kuwatunza, kuwasafishia nguo zenu, anawapeleka shuleni, akiwafundisha habari za Yesu, yawapasa kumheshimu mama mzuri huyo mwenye upendo kwa yote yaliyo ndani yenu. Yakupasa kumheshimu mwanamke huyo, naam, bwana, kwa sababu yeye ni mama halisi.

57 Wanazungumza juu ya kutojua kusoma na kuandika kwa wenyeji wa milima ya Kentucky. Mnaliona katika jambo hili ovu hapa. Baadhi yao mama wazee nje kule wangeweza kuja hapa Hollywood na kuwafundisha ninyi mama wa kisasa jinsi ya kuwalea watoto wenu. Hebu mtoto wake aingie usiku mmoja na nywele zake zimechafuliwa, na midomo...atoroke, (mnaitaje hiyo?) takataka ya kujipodolea wanayopaka usoni mwao, na nguo yake imebanwa upande mmoja, na amelala nje usiku kucha, amelewa, ndugu, atakata fimbo toka juu ya mti wa hickory naye hatatoka kwenda matembezini tena. Nawaambia, yeye ange ... Na kama ungekuwa na zaidi ya hao, ungekuwa na Hollywood nzuri zaidi hapa, na taifa zuri zaidi. Hiyo ni kweli. Ni kweli. "Jaribu tu kuwa wa kisasa," hiyo—hiyo ni moja ya hila za Ibilisi.

58 Sasa, msichana huyu mdogo, nilipomwangalia, moyo wangu ulitokwa na damu. Ndipo nikawaza, "Maskini jamaa mdogo."

Naye akasema, "Loo, unataka sigara, Billy?"

Nikasema, "La, mama." Nikasema, "Sivuti sigara."

Akasema, "Sasa, wewe ulisema huchezi dansi." Walitaka kwenda kwenye dansi nami nisingefanya hivyo. Kwa hiyo walisema kulikuwa na dansi chini kule, ambako wanakuita Bustani za Mikuyu.

Nami nikasema, "La, sichezi dansi."

Akasema, "Sasa, huchezi, huvuti sigara, hunywi pombe. Unajifurahisha vipi?"

Nikasema, "Vema, napenda kuvua samaki na napenda kuwinda." Hilo halikumvutia.

Kwa hiyo akasema, "Chukua sigara hii."

Nami nikasema, "La, mama, asante. Sivuti sigara."

59 Nami nilikuwa nimesimama kwenye madigadi ya gari. Walikuwa na ubao mrefu kwenye Ford za zamani, mnakumbuka, nami nilikuwa nimesimama kwenye ubao ule, tukaketi kwenye kiti cha nyuma mimi na yeye. Naye akasema, "Unamaanisha hutavuta sigara?" Kasema, "Na sisi wasichana tuna ujasiri mwingi kuliko ulionao."

Nikasema, "La, mama, siamini ninataka kufanya hivyo."

Akasema, "Ala, jike mkubwa wee!" Loo, jamani! Nilitaka kuwa Bill mkubwa mbaya, kwa hiyo mimi—mimi hakika sikutaka cho chote cha kike. Mnaona, nilitaka kuwa mwana ndondi mashuhuri, hilo lilikuwa kusudio la maisha yangu. Kwa hiyo nikasema ... "Jike! Jike!"

60 Singeweza kuvumilia jambo hilo, kwa hiyo nikasema, "Nipe hiyo!" Nikinyosha mkono wangu, nikasema, "Nitamwonyesha kama mimi ni jike au la." Nikachomoa sigara ile na nikaanza kuwasha kiberiti. Sasa, ninajua mnaninii ... Sasa, mimi siwajibiki kwa jambo mnalofikiria, wajibu wangu tu ni kuwaambieni kweli. Nilipoanza kuwasha sigara ile, nikiwa tu nimeamua kuivuta kama ninavyoamua kuitwaa Biblia hii, mnaona, nilisikia kitu kikifanya, "Whooooosssh!" Nilijaribu tena, sikuweza kuifikisha kinywani. Nami nikaanza kulia, nikatupa kitu hicho chini. Wakaanza kunicheka. Nikaondoka kwenda zangu nyumbani, nikapanda kwenda nikipitia shambani, nikaketi chini kule, nikalia. Na—na yalikuwa ni maisha ya kutisha sana.

61 Kumbuka siku moja Baba alikuwa akishuka kwenda mtoni pamoja na hao wavulana. Mimi na ndugu yangu, ilitubidi kuchukua mashua na kwenda huku na huko mtoni, tukitafuta chupa za kutilia chang'aa. Tulipata dazeni ya hizo kwa hela moja, kuziokota kando ya mto. Na Babangu alikuwa pamoja nami, naye alikuwa na moja ya zile chupa ndogo bapa...naamini zilikuwa chupa za kama nusu kibaba. Na kulikuwa na mti ulioangushwa na upepo, na Babangu... Basi mtu huyu alikuwa pamoja naye, Bw. Dornbush. Nilikuwa na ninii yake ... Alikuwa na mashua nzuri, nami nilitaka kufanya urafiki naye sababu nilitaka kutumia mashua ile. Ilikuwa na usukani mzuri na yangu haikuwa na usukani kabisa. Tulikuwa na mbao za zamani za kupigia makasia. Na kama angeniruhusu nitumie mashua hiyo ... Kwa hiyo, alikuwa akiunganisha vyuma hata akamtengenezea baba vyombo vya kutengenezea chang'aa. Kwa hiyo yeye ... Walinyosha miguu yao kulingama mti ule, kisha Babangu akaingiza mkono katika mfuko wake wa nyuma akachomoa chupa ndogo bapa ya chang'aa, akampa naye akanywa kidogo, akamrudishia Babangu naye akanywa kidogo, na akaiweka chini kwenye chipukizi dogo kando ya mti ulioanguka. Naye Bw.Dornbush akaichukua, akasema, "Haya basi, Billy."

Nikasema, "Asante, sinywi pombe."

Akasema, "Mbranham, na hunywi?" Kila mmoja wao alikufa kiume, karibu kila mmoja. Naye akasema, "Mbranham, na eti hunywi?"

Nikasema, "La, bwana."

"La," baba akasema, "nilizaa jike moja."

62 Babangu aniite jike! Nikasema, "Nipe hiyo chupa!" Nikafungua kile kizibo, nimeamua kuinywa, bali nilipoanza kuitia kinywani, "Whooooosssh!" Nikairudisha ile chupa nikatimua mbio nikishuka kupitia kwenye shamba nikienda kasi nilivyoweza, huku ninalia. Kitu fulani kisingeniruhusu nifanye hivyo. Mnaona? Nisingeweza kusema kwamba nilikuwa mwema kwa vyo vyote (nilikuwa nimeamua kulitenda), bali ni Mungu, neema, neema ya ajabu ambayo ilinizuia nisitende mambo hayo. Nilitaka kuyatenda, mimi mwenyewe, bali Yeye asingeniruhusu niyatende.

63 Baadaye nikapata msichana nilipokuwa na umri wa kama miaka ishirini na miwili, alikuwa kipenzi. Alikuwa msichana ambaye alienda kanisani, Mluteri wa Kijerumani. Jina lake lilikuwa Brumbach, B-r-u-m-b-a-c-h, linatokana na jina la Brumbaugh. Naye alikuwa msichana mzuri. Hakuvuta wala kunywa, au—au hakucheza dansi au cho chote kile, msichana mzuri. Nilifuatana naye kwa kipindi kidogo, nami ninge ... Halafu, kama miaka ishirini na miwili, nilikuwa nimekusanya fedha za kutosha hata nikajinunulia Ford kuukuu, nami...tungeenda kuonana pamoja. Na kwa hiyo, wakati ule, hapakuwa na kanisa la Kiluteri lililo karibu, walihama toka Howard Park juu kule.

64 Na kwa hiyo kulikuwa .. mhudumu, yule aliyenitawaza kwenye kanisa la Kimisionari la Kibatisti, Daktari Roy Davis. Dada Upshaw, yule hasa aliyempeleka Ndugu Upshaw kwangu, au aliyezungumza naye kunihusu mimi, Daktari Roy Davis. Na kwa hiyo alikuwa akihubiri, na alikuwa ana kanisa la Kwanza la Kibatisti, au ile—ile...Siamini lilikuwa kanisa la Kwanza la Kibatisti, mojawapo, lilikuwa la Kimishenari... liitwalo kanisa la Kimishenari la Kibatisti kule Jeffersonville. Naye alikuwa akihubiri mahali hapo wakati huo, nasi tungeenda kanisani usiku, kwa hiyo ... nasi tungerudi. Nami kamwe sikujiunga na kanisa, bali nilipenda tu kwenda pamoja naye. Kwa sababu wazo kuu lilikuwa ni "kwenda pamoja naye," afadhali niwe mwaminifu.

65 Kwa hiyo basi nikaenda pamoja naye, na siku moja mimi ... Alikuwa ametoka kwenye familia nzuri. Basi nilianza kufikiri, "Unajua, unajua, hainipasi kupoteza wakati wa msichana yule. Siyo—siyo sawa, kwa sababu ni msichana mzuri, na mimi ni maskini na—na mimi..." Baba yangu alikuwa na afya mbaya, nami—nami... Hapakuwepo na njia kwangu mimi kumtunza msichana kama yule, ambaye amezoea nyumba nzuri na mazulia sakafuni.

66 Ninakumbuka zulia la kwanza nililopata kuona, sikujua lilikuwa ni kitu gani. Nilipitia kando yake. Nilifikiria lilikwa kitu kizuri sana nilichowahi kuona maishani mwangu. "Wangewekaje kitu kama hicho

sakafuni?" Ilikuwa ni zulia la kwanza nililopata kuona. Lilikuwa—lilikuwa moja ya haya ... Naamini linaitwa "mazulia yaliyosukwa." Naweza nikosee hilo. Aina fulani ya kama "kirago" au kitu fulani kilichosukwa pamoja, na kulazwa sakafuni. Zulia zuri la kijani na nyekundu, na waridi kubwa lililochorwa katikati yake, mnajua. Kilikuwa kitu cha kupendeza sana.

67 Na kwa hiyo ninakumbuka ni—niliamua kwamba au ilinibidi kumwomba nimuoe, au itanilazimu niondoke na kuacha mtu anayefaa amuoe, mtu ambaye angekuwa mzuri kwake, ambaye angeweza kumtunza na angekuwa mwema kwake. Ningeweza kuwa mwema kwake, bali ni—ni—nilikuwa tu ninapata senti ishirini kwa saa. Kwa hiyo nisingeweza kupata fedha za kutosha kumtunza vizuri. Nami ... Tukiwa na jamaa yote hiyo tuliyopaswa kutunza, na Babangu amekuwa na afya mbaya, basi ilinibidi mimi kuwatunza wote, kwa hiyo nilikuwa na wakati mgumu kweli.

68 Kwa hiyo nikawaza, "Vema, jambo pekee kwangu kufanya ni kumwambia ya kwamba ni—ni ... yeye ... Mimi—sitarudi, kwa sababu nilimthamini mno nisingetaka kuharibu maisha yake na kumwacha apoteze wakati akinifuata mimi." Halafu niliwazia, "Kama mtu fulani angeweza kumpata na kumuoa, awe na nyumba nzuri. Na labda kama nisingeweza kumpata, ninge—ningejua kwamba alikuwa na furaha."

Na kwa hiyo niliwazia, "Bali mimi—mimi si—siwezi kumwacha!" Nami ni—nilikuwa katika hali mbaya sana. Na siku baada ya siku ningewazia jambo hilo. Kwa hiyo niliona haya sana nisingemwomba nimuoe. Kila usiku ningeamua, "Nitamwomba." Na, wakati mimi, ah, ni kitu gani kile, vipepeo, au kitu fulani unachopata katika...? Ninyi ndugu wote huko nje labda mlikuwa na tukio lile lile katika jambo hilo. Na hali fulani halisi ya ajabu, uso wangu ungepata joto. Si—sikujuu. Nisingeweza kumwuliza.

Kwa hiyo nadhani unashangaa jinsi nilivyopata kuoa. Unajua nini? Nilimwandikia barua nikamwomba. Na kwa hiyo yeye ... Sasa, haikuwa "Bi mpendwa," ilikuwa zaidi kidogo (mnajua) upande wa mapenzi kuliko hilo. Haikuwa tu ma—mapatano, ilikuwa... Ni—niliandika vizuri sana nilivyoweza.

69 Nami nilimwogopa mama yake kidogo. Mama yake alikuwa ... alikuwa kwa namna fulani mkali. Na, lakini baba yake alikuwa mzee mpole wa Kidachi, mzee mzuri tu. Alikuwa msimamizi wa udugu na wafanya kazi wa garimoshi kwenye njia ya reli, akipokea kama dola mia tano kwa mwezi kwenye zama hizo. Na mimi nikifanya senti ishirini kwa saa, kumwoa binti yake. A-ha! Nilijua nisingefanikiwa kabisa. Na mama yake alikuwa ... Sasa, yeye ni mama mzuri. Na yeye—yeye alikuwa kwa namna fulani mmoja wa hawa watu wa tabaka ya juu, mnajua, kama mwenye kisirani, mnajua, na kwa hiyo sikumfaa kitu kwa vyo vyote. Nilikuwa tu maskini kijana mshamba asiye na mbele wala nyuma, naye alifikiria Hope anapaswa kuambatana na mvulana wa tabaka bora zaidi, nami na—na—nafikiri alikuwa sahihi. Na kwa hiyo ... Lakini si—sikuwazia jambo hilo wakati huo.

70 Kwa hiyo nikawaza, "Vema, sasa, sijui vipi. Si—siwezi kumwomba baba yake, na ni—nina hakika sitamwomba mama yake. Na kwa hiyo yanibidi nimwombe yeye kwanza." Kwa hiyo nikaandika barua. Na asubuhi ile njiani nikienda kazini, niliitumbukiza kwenye sanduku la barua. Sanduku la barua ... Tulikuwa tunaenda kanisani Jumatano usiku, na hiyo ilikuwa Jumatatu asubuhi. Nilijaribu Jumapili nzima kumwambia kwamba nilitaka kuoa, nami sikuweza kabisa kupata ujasiri wa kutosha.

Kwa hiyo basi niliitumbukiza kwenye sanduku la barua. Basi huko kazini siku hiyo nikawaza, "Na mama yake akiipata ile barua je?" Loo, jamani! Ndipo nilijua nitajuta kama—kama akiwahi kuipata, sababu hakunijali sana. Naam, nilikuwa nikiwazia na kuliwazua tu jambo hilo.

71 Na Jumatano ile usiku nilipokuja, loo, jamani, nikawaza, "Hivi nitaendaje kule juu? Iwapo mama yake aliipata barua ile kweli atanishambulia, kwa hiyo natumaini yeye aliipata." Niliandika kwenye bahasha "Hope." Hilo ndilo lililokuwa jina lake, Hope. Na kwa hiyo nilisema, "Nitaiandika tu juu hapa Hope." Na kwa hiyo ... Na nalifikiri labda yawezekana hakuipata.

Kwa hiyo nilijua vyema kuliko kusimama nje na kupiga honi kusudi yeye atoke. Loo, jamani! Na mvulana ye yote ambaye hana ujasiri wa kutosha kutembea hadi nyumbani na kubisha mlangoni na kumwomba msichana, haimpasi kamwe kutoka naye nje kwa vyo vyote. Hiyo ni kweli kabisa. Huo ni upuzi mkubwa sana. Hiyo ni tabia duni.

72 Na kwa hiyo nilisimamisha Ford yangu kuukuu, mnajua, na nilikuwa nimeisafisha vizuri sana. Na kwa hiyo nikapanda na kubisha mlangoni. Salala, mama yake akaufungua mlango! Ilikuwa vigumu kwangu kupumua, nikasema, "U—u—u hali gani, Bibi Brumbach?" Naam.

Akasema, "U hali gani, William."

Nikawaza, "A-ha, 'William'!"

Na—naye akasema, "Je! Utaingia?"

Nikasema, "Asante." Nikaingia mlangoni. Nikasema, "Hope yuko tayari?"

Mara tu huyu hapa Hope anapita upesi mle nyumbani, msichana tu wa umri upatao miaka kumi na

sita. Naye akasema, "Halo, Billy!"

Nami nikasema, "Halo, Hope." Kisha nikasema, "Uko tayari kwenda kanisani?"

Akasema, "Hebu kidogo."

Nikawaza, "Loo, jamani! Yeye hakuipata. Yeye hakuipata. Sawa, sawa, sawa. Wala hata Hope hajaipata, kwa hiyo itakuwa barabara, sababu angeliigusia kwangu." Kwa hiyo nilijisikia mzuri sana.

73 Na halafu nilipotoka kanisani, ikawa nikawaza, "Vipi kama aliipata?" Mnaona? Basi sikuweza kusikia ambacho Daktari Davis alikuwa anasema. Nikamtazama, nikawaza, "Kama pengine analinyamazia jambo hilo, na kwa kweli atanikaripia nitakapotoka hapa, kwa kumwomba yeye jambo hilo." Nami sikuweza kusikia yale Ndugu Davis aliyokuwa akisema. Na—nami nikamtazama, nikawaza, "Lahaula, ninachukia kumwacha, lakini... Na mimi—mimi...ukweli hakika utajidhihirisha."

Kwa hiyo baada ya ibada tukaanza kutembea tukishuka barabarani pamoja, tukienda nyumbani, na—na kwa hiyo tulitembea hadi kwenye ile Ford kuukuu. Na huko njiani kote mbalamwezi inawaka kwelikweli, mnajua, nikamwangalia naye alikuwa mzuri kweli. Jamani, ningemwangalia, na kuwaza, "Lo, jinsi ningefurahi kumpata, bali nafikiri siwezi."

74 Na kwa hiyo nilitembea mbele zaidi, mnajua, na ningemwangalia tena. Nikasema, "Una—unajisikiaje usiku wa leo?"

Akasema, "Loo, niko sawa."

Nasi tukasimamisha ile Ford kuukuu chini na tukaanza kutoka, mnajua, kuzunguka kando, kutembea kuzunguka kona na kuelekea nyumbani kwao. Na nilikuwa ninapanda kuelekea mlangoni pamoja naye. Nikawaza, "Unajua, labda hakuipata kamwe ile barua, kwa hiyo afadhali nisahau jambo hilo tu. Nitakuwa na juma lingine la neema hata hivyo." Kwa hiyo nikajisikia vizuri sana.

Akasema, "Billy?"

Nikasema, "Naam."

Akasema, "Nimepata barua yako." Loo, jamani!

Nikasema, "Uliipata?"

Akasema, "A-ha." Vema, yeye aliendelea tu kutembea, hakusema neno lingine.

Nikawaza, "Mwanamke, niambie jambo fulani. Nifukuze au uniambie unachowazia juu ya jambo hilo." Ndipo nikasema, "Uli—uliisoma?"

Akasema, "A-ha."

Jamani, mnajua jinsi mwanamke anavyoweza kukutia wasiwasi. Loo, si—sikumaanisha hilo namna hiyo, mnaona. Mnaona? Bali, hata hivyo, mnajua, ni—niliwaza, "Kwa nini usiseme kitu?" Mnaona, basi nikazidi kusonga mbele. Nikasema, "Uliisoma yote?"

Naye ... [Sehemu tupu kwenye kanda — Mh.] "A-ha."

75 Kwa hiyo tulikuwa tunakaribia mlangoni, nami nikawaza, "Jamani, usinifikishe kwenye baraza, sababu singeweza kuwatoroka, kwa hiyo niambie sasa." Na kwa hiyo nikaendelea kungojea.

Naye akasema, "Billy, ningependa kufanya hivyo." Akasema, "Ninakupenda." Mungu aibariki nafsi yake sasa, yuko Utukufuni. Akasema, "Ninakupenda." Kasema, "Nafikiri yatubidi kuwaambia mzazi wetu, wazazi kuhusu jambo hilo. Unaonaje?"

Ndipo nikasema, "Mpenzi, sikiliza, hebu na tuanze jambo hili kwa pendekezo la nusu kwa nusu." Nikasema, "Nitamwambia baba yako kama utamwambia mama yako." Nikijiondolea sehemu iliyo nzito na kumwelekezea, kwanza.

Akasema, "Sawa, iwapo utamwambia Baba kwanza."

Nikasema, "Vema, nitamwambia Jumapili usiku."

76 Na kwa hiyo usiku wa Jumapili ukafika, nikamleta nyumbani kutoka kanisani na mimi... Aliendelea kunitazama. Ndipo niliangalia, na ilikuwa saa tatu u nusu, wakati wangu wa kuondoka umewadia. Kwa hiyo Charlie alikuwa ameketi mezani mwake, akitumia mashine ya kupiga chapa. Bibi Brumbach ameketi pembeni, akifuma, mnajua, au vijigurudumu unavyoweka juu ya vitu, mnajua. Sijui mnaziitaje Na kwa hiyo alikuwa akifanya vitu kama hivyo. Basi Hope aliendelea kuniangalia, naye angenikunjia uso, mnajua, akielekeza kwa baba yake. Nami ... Loo, jamani! Nikawaza, "Vipi kama akisema, 'La'?" Kwa hiyo nikaanza

kwenda mlangoni, nikasema, "Vema, nadhani afadhali niende."

77 Basi nikaenda mlangoni, na—na akaanza kwenda mlangoni pamoja nami. Yeye daima angekuja mlangoni na kuniambia "usiku mwema." Kwa hiyo nikaanza kwenda kuelekea mlangoni, naye akasema, "Hutamwambia?"

Nami nikasema, "A-ha!" Nikasema, "Hakika ninajaribu kufanya hivyo, lakini si—si—sijui jinsi nitakavyofanya jambo hilo."

Naye akasema, "Nitarudi tu na utamwita atoke." Kwa hiyo akarudi nyuma na kuniacha nimesimama pale.

Nami nikasema, "Charlie."

Akageuka na kusema, "Naam, Bill?"

Nikasema, "Naweza kuzungumza nawe kwa dakika moja tu?"

Akasema, "Hakika." Akageuka kutoka kwenye dawati lake. Bibi Brumbach alimwangukia, akamwangukia Hope, kisha akanitazama.

Ndipo nikasema, "Tafadhali uje nje barazani."

Naye akasema, "Naam, nitatoka." Kwa hiyo akatoka akaja barazani.

Nikasema, "Hakika ni usiku mzuri sana, sivyo?"

Naye akasema, "Ndiyo, ni mzuri."

Nikasema, "Hakika kumekuwa joto."

"Bila shaka," akaniangukia.

Nikasema, "Nimekuwa nikifanya kazi sana," nikasema, "unajua, hata mikono yangu imepata sugu."

Akasema, "Unaweza kumchukua, Bill." Loo, jamani! "Unaweza kumchukua."

78 Nikawaza, "Loo, hilo ni bora zaidi." Nikasema, "Unamaanisha kweli, Charlie?" Yeye alisema ... Nikasema, "Charlie, angalia, ninajua ya kwamba yeye ni binti yako, nawe una pesa."

Naye akaunyosha mkono wake akanishika mkono. Akasema, "Bill, sikiliza, hela siyo mambo yote yaliyo katika maisha ya binadamu." Yeye alisema ...

Nikasema, "Charlie, ni—ninapata senti ishirini tu kwa saa, bali ninampenda naye ananipenda. Nami ninakuahidi, Charlie, kwamba nitafanya kazi mpaka hizi...mpaka sugu ziondoke mikononi mwangu, nipate kumtunza. Nitakuwa mwaminifu kwake niwezavyo kuwa."

Akasema, "Ninaamini jambo hilo, Bill." Akasema, "Sikiza, Bill, ninataka kukwambia." Kasema, "Unajua, furaha, kwa jumla haihitaji hela kuwa na furaha. Kasema, "Uwe tu mwema kwake. Nami ninajua utafanya hivyo."

Nikasema, "Asante, Charlie. Hakika nitafanya hivyo."

Ndipo ulikuwa wakati wake wa kumwambia Mama. Sijui jinsi gani alifaulu, bali tulioana.

79 Kwa hiyo, tulipooana, hatukuwa na kitu, hakuna cho chote cha kununulia vyombo vya nyumbani. Nafikiri tulikuwa na dola mbili ama tatu. Kwa hiyo tulikodi nyumba, ilitugharimu dola nne kwa mwezi. Kilikuwa kijumba kidogo, cha zamani chenye vyumba viwili. Na mtu fulani alitupa kitanda cha kale cha kukunja. Sijui kama kuna mtu ye yote aliyewahi kuona kitanda cha kale cha kukunja? Na wakatupa sisi hicho. Kisha nikashuka kwenda kwa Sears na Roebucks nikanunua meza ndogo na viti vinne, na ha—haikupakwa rangi, mnajua, nasi tuliipata hiyo kwa wakati mzuri. Na kwa hiyo basi nilikwenda kwa Bw. Weber, mfanya biashara wa vyombo vikuukuu, nikanunua jiko la kupikia. Nililipa senti sabini na tano, na dola moja na kitu kununulia nondo zake. Tukaweka vyombo vya nyumbani. Nakumbuka nilipovichukua vile viti na kuvichora mmea wa shamrock, nilipokuwa nikivipaka rangi. Na, loo, tulikuwa na furaha, hata hivyo. Tulikuwa pamoja, kwa hiyo hilo ndilo lililokuwa la lazima. Naye Mungu, kwa rehema Yake na wema Wake, tulikuwa mume na mke wachanga wenye furaha sana duniani.

Niliona hili, kwamba furaha haipo katika kiasi ulicho nacho cha mali ya ulimwengu, bali ni jinsi ulivyoridhika na sehemu ambayo umegawiwa.

80 Na, baada ya kitambo kidogo, Mungu akashuka akaja akabariki nyumba yetu ndogo, tukapata mtoto mwanamume. Jina lake lilikuwa Billy Paul, yuko kwenye ibada sasa hivi hapa. Na baadaye kidogo tokea hapo, kama miezi kumi na mmoja, Yeye alitubariki tena na mtoto wa kike jina lake Sharon Rose,

lililotokana na neno "Waridi la Uwandani."

Basi nakumbuka siku moja nilikuwa nimeweka akiba fedha zangu na nilikuwa nataka kwenda likizoni, niende mahali fulani, Ziwa Paw Paw, kuvua samaki. Na nilipokuwa nikirudi ...

81 Na katika wakati huu ... Ninaacha kuongoka kwangu. Nilikuwa nimeongoka. Na nilitawazwa na Daktari Roy Davis, katika kanisa la Kimishenari la Kibatisti, na nilikuwa mhudumu na nina Maskani ambayo sasa ninahubiria kule Jeffersonville. Nami nilikuwa mchungaji kwenye hilo kanisa dogo. Nami ...

Hakuna fedha, nilifanya kazi ya uchungaji kwenye kanisa lile miaka kumi na saba na kamwe sikupata hata senti moja. Sikuamini katika ku- ... Hapakuwa hata na sahani ya sadaka ndani yake. Na fungu la kumi ambalo nilipata kutokana na ile kazi, na kadhalika, kulikuwa na sanduku dogo nyuma ya jengo, yalisema, maandishi yaliyokuwepo juu yake, "Kadiri mlivyowatendea mmojawapo wa hao walio wadogo Wangu, mlinitendea Mimi." Na halafu hivyo ndivyo kanisa lilivyolipiwa. Tulikuwa na mkopo wa miaka kumi kulilipia, na lililipiwa chini ya miaka miwili. Nami kamwe sikuchukua sadaka ya namna yo yote.

Na halafu nilikuwa, loo, na dola chache nilizoweka akiba kwa ajili ya likizo yangu. Mke wangu alifanya kazi, pia, kwenye Kiwanda cha Fine Shirt. Msichana mzuri mpenzi. Na kaburi lake labda lina theluji leo hii, bali yeye bado yuko moyoni mwangu. Nami ninakumbuka wakati alifanya kazi sana kunisaidia kupata fedha za kutosha kwenda kwenye ziwa hili kuvua samaki.

82 Na nilipokuwa ninarudi kutoka ziwani, nikaanza kuona, nikija Mishawaka na South Bend, Indiana, basi nikaanza kuona magari ambayo yalikuwa na maandishi upande wa nyuma, yakisema, "Yesu Pekee." Ndipo nikawazia, "Hilo linaonekana geni, 'Yesu Pekee.'" Basi nikaanza kuona yale maandishi. Na yalikuwa juu ya kila kitu tokea baiskeli, Ford, Kadilak, na kadhalika, "Yesu Pekee." Basi nikafuatilia baadhi yao kule chini, nao wakafika kwenye kanisa kubwa mno. Nami niliona walikuwa Wapentekoste.

Nilikuwa nimesikia kuhusu Wapentekoste, bali walikuwa kundi la "watakatifu wanaojifingirisha ambao walijitupa sakafuni na kutoka povu vinywani mwao," na kila kitu ambacho waliniambia kuwahusu. Kwa hiyo sikutaka kuhusiana nao.

Kwa hiyo niliwasikia wote wakiendelea na mambo yao mle, nami nikawaza, "Naona nitaingia ndani." Kwa hiyo nilisimamisha Ford yangu kuukuu nikaingia, na kuimba kwote ulikowahi kusikia maishani mwako! Nami nikatambua kulikuwa na makanisa makubwa mawili, mojawapo lilitwa P.A la J.C., na P.A. la W., wengi wenu ninyi watu mwaweza kukumbuka madhehebu hayo ya zamani... Nafikiri yameungana, sasa yanaitwa, yanaitwa kanisa la United Pentekostal. Vema, niliwasikiliza baadhi ya waalimu wao. Nao walikuwa wakisimama pale, loo, walikuwa wakifundisha kuhusu Yesu na jinsi Yeye alivyokuwa Mkuu, na jinsi kila kitu kilivyokuwa kikuu, na kuhusu "ubatizo wa Roho Mtakatifu." Nikawaza, "Wanazungumzia nini?"

83 Na, baada ya kitambo kidogo, mtu fulani aliruka na kuanza kunena kwa lugha. Vema, sijapata kusikia kitu kama hicho maishani mwangu. Na hapa akaja mwanamke fulani anakimbia mbio sana awezavyo. Halafu wote wakasimama wakaanza kukimbia. Basi nikawaza, "Naam, ndugu, hakika hawana taratibu za kanisa!" Wakipiga yowe na kupaza sauti na kufanya vurugu, nikawaza, "Kundi gani hili!" Lakini, mnajua, jambo fulani kuhusu hilo, kadiri nilivyoendelea kuketi pale, ndivyo nilivyozidi kulipenda. Kulikuwa na kitu kilichoonekana ni kizuri sana. Nami nikaanza kuwaangalia. Na ikaendelea. Nikawaza, "Nitavumilia tu kwa muda kidogo, maana nita- ... Niko karibu na mlango. Kama likianza jambo la hatari, nitakimbia nje. Najua mahali gari langu dogo limeegeshwa, hapa pembeni tu."

84 Basi nikaanza kusikia baadhi ya hao wahubiri, walikuwa wasomi na wanafunzi. Mbona, nikawaza, "Hilo ni zuri."

Kwa hiyo ukaja wakati wa chakula cha jioni, wakasema, "Kila mtu amealikwa kwenye chakula cha jioni."

Lakini niliwazia, "Ngoja kidogo. Nina dola na senti sabini na tano za kwenda nyumbani, nami ..." Hizo ndizo tu nilizokuwa nazo kwa fedha ya petroli. Nilichukua hizo tu kunifikisha nyumbani. Nami nilikuwa na Ford yangu ya kale, ilikuwa ni Ford nzuri ya kale. Haikuwa mbovu, ilikuwa tu kama hii hapa nje, ila tu imechakaa. Na hiyo ... Kwa kweli niliamini Ford ile ingeenda maili thelathini kwa saa, bali bila shaka hizo zilikuwa kumi na tano upande *huu* na kumi na tano upande *huu*. Mnaona, ukiziweka pamoja, una thelathini. Na kwa hiyo hiyo ... Nikawaza, "Vema, usiku ule nafikiri nitatoka nje na baada ya ile..." Nilikuwa nangoja ibada ya usiku.

85 Na, loo, yeye alisema, "Wahubiri wote, bila kujali madhehebu, njoni jukwaani." Naam, tulikuwa kama watu mia mbili juu pale, nikapanda juu. Na kwa hiyo akasema, "Sasa, hatuna muda wa kutosha kwenu nyote kuhubiri." Akasema, "Pita tu na useme wewe ni nani na unatoka wapi."

Vema, wakati wangu ulifika, nikasema, "William Branham, Mbatisti. Jeffersonville, Indiana." Nikapita.

Ningewasikia hao wengine wote wakijiita wenyewe, "Pentekoste, Pentekoste, Pentekoste, P.A. ya

W., P.A.J.C., P.A.W., P ...”

Nikapita. Nikawaza, “Naam, nadhani mimi ndiye mgeni asiye na mwenziwe.” Kwa hiyo nikaketi chini, nikangojea.

86 Na, siku ile, walikuwa na wahubiri wazuri, vijana mbele pale, nao walihubiri kwa nguvu. Na halafu wakasema, “Mtu atakayeleta ujumbe usiku wa leo ni ...” Ninaamini walimwita, “Mzee.” Nao wahudumu wao, badala ya “Kasisi,” ilikuwa ni “Mzee.” Nao wakamleta mzee mweusi pale, naye alikuwa na moja ya makoti haya ya mhubiri ya mtindo wa kale. Sidhani mmewahi kuona moja. Mkia mrefu wa njiwa nyuma, mnajua, lenye ukosi wa mahameli, naye alikuwa na kishungi kidogo tu cha mvi kinachozunguka kichwa chake. Maskini mzee huyo, alikuja namna *hii*, mnajua. Naye akasimama pale kisha akageuka. Na ambapo wahubiri wote walikuwa wakihubiri kuhusu Yesu na mambo makuu...jinsi Yeye alivyo mkuu, na kadhalika, yule mzee alichukua fungu lake la maneno kutoka katika Ayubu. “Ulikuwa wapi nilipoiweka misingi ya nchi, au hapo nyota za asubuhi zilipoimba pamoja na Wana wa Mungu walipopiga kelele kwa furaha?”

Na maskini mzee yule, nikawaza, “Kwa nini hawakuweka baadhi ya hao vijana juu kule kuhubiri?” Kuu...mahali pale palijaa watu hata wakasongamana. Nami nikawaza, “Kwa nini hawakufanya hivyo?”

87 Kwa hiyo basi huyu mzee, badala ya kuhubiri yaliyokuwa yakiendelea humu duniani, alianza kuhubiri yaliyokuwa yanatendeka Mbinguni wakati wote. Naam, alimchukua Yeye pale mwanzo pale mwanzo wa wakati, kisha akamrudisha Yeye kwenye Kuja mara ya Pili akishuka chini kwenye upinde wa mvua. Mbona, sijapata kusikia mahubiri kama hayo maishani mwangu! Yapata wakati huo Roho akamjilia, akaruka urefu kama *huu* huku anagongesha visigino vyake pamoja, akatupa mabega yake nyuma akajifiringisha pale jukwaani, kasema, “Hamna nafasi ya kutosha hapa kwangu mimi kuhubiria.” Naye alikuwa na nafasi kubwa kuliko niliyo nayo hapa.

Nikawaza, “Iwapo Kitu hicho kitamfanya mzee atende jinsi hiyo, je kingefanya nini kama Chenyewe kingenipata mimi?” Ni—nikawaza, “Labda ninahitaji sehemu ya kitu Hicho.” Mbona, alitoka hapa, nikamsikitikia jamaa yule mzee. Bali, alipoondoka, nilikuwa ninajisikitikia. Nami nilimtaazama akiondoka pale.

88 Nilitoka usiku ule, nami nikawaza, “Sasa, asubuhi inayofuata sitamruhusu mtu ye yote ajue wapi, mimi ni nani.” Kwa hiyo nikaondoka nikaenda, na usiku ule nilinyosha suruali yangu. Nilichukua ile... nilikwenda kwenye shamba la mahindi kulala, nami nikashuka kwenda kujinunulia sambusa zilizochacha. Ninyi ... Nilinunua fungu zima kwa hela moja. Kulikuwa na bomba la maji chini pale, nikachota maji kidogo. Kwa hiyo nilijua kwamba hizo zingenichukua muda kidogo, kwa hiyo nikachukua maji nikanywa, nikaondoka nikala sambusa zangu. Kisha nikarudi nikanywa maji tena. Nikaenda kwenye shamba la mahindi, nikachukua viti viwili na kulaza suruali yangu ndogo ya pamba yenye milia mle ndani, nikaibana niinyoshe kwa kiti.

Na, usiku huo, niliomba karibu usiku kucha. Nikasema, “Bwana, kitu gani hiki nimekutana nacho? Sijawahi kuona watu wa kidini kama hao maishani mwangu.” Kisha nikasema, “Nisaidie kujua maana ya haya yote.”

89 Na asubuhi iliyofuata nilishuka nikaenda kule. Tulikaribishwa kifunguakinywa. Bila shaka, nisingekuja kula pamoja nao, kwa sababu sikuwa na kitu cha kutolea sadaka. Nami nikarudi tu. Na asubuhi iliyofuata nilipoingia, mbona (nimekula sambusa zangu), basi nikakaa chini. Na mmoja wao alikuwa kwenye maikrofoni. Nami sijawahi kuona maikrofoni hapo kabla, na niliogopa kitu hicho. Kwa hiyo wao ... Na ilikuwa na kamba ndogo inayoning'inia hapa juu, nayo ikining'inia chini. Moja ya hizo maikrofoni za kushusha, namna hiyo. Naye akasema, “Jana usiku, jukwaani, kulikuwako na mhubiri kijana hapa, Mbaptisti.”

Nikawaza, “A-ha, watanipa kazi kubwa sasa.”

Naye alisema, “Yeye alikuwa mhubiri mdogo kuliko wote kwenye jukwaa. Jina lake lilikuwa Branham. Kuna mtu ye yote anayejua aliko? Mwambie aje, tunamtaka alete ujumbe wa asubuhi.”

90 Loo, jamani! Nilikuwa nimevaa T-shati, suruali ya pamba yenye milia, unajua. Nasi Wabatisti tunaamini yakubidi uvae suti, upate kwenda mimbarani, mnajua. Kwa hiyo ... Na mimi—mimi nilikaa kimya kabisa. Na katika wakati huo ... Waliufanyia huko Kaskazini wakati huo sababu (mkutano wao wa kimataifa) watu weusi hawangeuhudhuria kama ulifanyiwa huko Kusini. Walikuwa na watu weusi pale, nami nilikuwa wa Kusini, nilikuwa na kiburi bado, mnaona, nilifikiri nilikuwa bora kuliko mtu mwingine. Na ilitokea kuwa asubuhi ile, papo hapo karibu nami aliketi m—mtu mweusi. Kwa hiyo niliketi nikamwangalia. Nikawaza, “Vema, yeye ni ndugu.”

Naye akasema, “Kuna mtu anayejua mahali alipo William Branham?” Nikainama chini kitini namna *hii*. Kwa hiyo akasema, akalitangaza mara ya pili, kasema, “Kuna mtu huko nje” (akavuta ndani hii mikrofone ndogo) “ajuaye alipo William Branham? Mwambie tunamtaka aje jukwaani atoe ujumbe wa asubuhi. Yeye ni mhubiri wa Kibatisti kutoka Indiana ya kusini.”

91 Nilikaa kimya kabisa na kuinama chini, unajua. Hakuna mtu aliyenijua, kwa vyo vyote. Yule mvulana

mweusi akaniangalia, akasema, "Je, wewe unajua aliko?"

Niliwaza. Mimi—mimi aidha itanilazimu kudanganya au kufanya jambo fulani. Kwa hiyo nikasema, "Inama hapa chini."

Akasema, "Naam, bwana?"

Nikasema, "Ninataka kukwambia jambo fulani." Nikasema, "Mimi—mimi ndiye."

Akasema, "Vema, nenda kule juu."

Nami nikasema, "La, siwezi. Mnaona," nikasema, nimevaa suruali hii ndogo kuukuu ya pamba yenye milia na T-shati hii ndogo." Nikasema, "Nisingeweza kwenda kule."

Akasema, "Hao watu hawajali jinsi unavyovalia. Nenda huko juu."

Nikasema, "La, la." Nikasema, "Nyamaza kimya, usiseme kitu sasa."

Nao wakaja tena kwenye maikrofoni baada ya kitambo kidogo, kasema, "Kuna mtu anayejua aliko William Branham?"

Akasema, "Huyu hapa! Huyu hapa! Huyu hapa!" Loo, jamani! Hapo nilisimama nikiwa nimevaa hiyo fulana ndogo, mwajua. Na hapa mimi ...

92 Akasema, "Njoo huku, Bw. Branham, tunataka ulete ujumbe." Loo, jamani, mbele ya hao wahubiri wote, a-ha, watu hao wote! Basi nikaenda haraka, mnajua. Uso wangu umeiva, na masikio yangu yakiwasha. Basi nikaenda haraka kule juu, suruali ya pamba yenye milia, na T-shati, mhubiri, mhubiri wa Kibatisti akienda kwenye maikrofoni, hajaona moja hapo awali, mnaona.

Ndipo nikasimama pale, nikasema, "Vema, si—si—sijui kuhusu jambo hili." Nilikuwa nikihangaika, wasiwasi kweli, mnajua. Ba—basi nikafungua hapa katika Luka 16, nami nikawaza, "Vema, sasa..." Ndipo ni—nikapata somo, Basi akayainua macho yake kuzimuni, ndipo akalia. Nikapata... Kwa hiyo ni—nikaanza kuhubiri, unajua, basi nilipoanza kuhubiri nikajisikia afadhali kidogo. Nami nikasema, "Yule tajiri alikuwa kuzimuni, basi akalia." Hayo maneno madogo matatu, kama nilivyo na mahubiri mengi kama hayo, "Wewe Unaamini Hili," na "Nena na Mwamba," mmenisikia mimi nikiyahubiri. Nami nilikuwa na, "Ndipo akalia." Nami nikasema, "Hakuna watoto kule, hakika siyo huko kuzimuni. Ndipo akalia." Nikasema, "Hakuna maua kule. Kisha akalia. Hakuna Mungu kule. Kisha akalia. Hakuna Kristo kule. Kisha akalia." Ndipo nikalia. Kitu fulani kilinishika. Jamani! Loo, jamani! Baadaye, sijui kilichotukia. Basi nilipopata kujirudia, nilikuwa nimesimama kule nje. Hao watu walipiga yowe na kupaza sauti na kulia, pamoja nami, tulikuwa na wakati wa ajabu sana.

93 Nilipotoka nje alitokea mtu aliyenijia huku amevaa kofia kubwa ya Texas, buti kubwa, akanijia, kasema, "Mimi ni Mzee *fulani wa fulani*." Mhubiri, buti za cowboy, amevaa nguo za cowboy.

Nikawaza, "Vema, suruali yangu ya pamba yenye milia siyo mbaya basi."

Kasema, "Nataka wewe uje huko chini Texas ukanifanyizie uhamsho."

"A-ha, hebu niandike hilo, bwana." Nami nikaliandika namna hiyo.

Hapa akaja mtu akiwa amevaa moja ya namna ya hizi suruali ndogo za mpira wa gofu, hapo walipozoea kucheza gofu, mnajua, walikuwa wanavaa suruali ndogo fupi. Akasema, "Mimi ni Mzee *Fulani* kutoka Miami. Ninapenda kuninii ..."

Nikafikiri, "Jamani, pengine mavazi si jambo kubwa." Nikalingalia, na nikawaza, "Vema."

94 Kwa hiyo nikanyakua vitu hivi, na huyoo nikaenda zangu nyumbani. Mke wangu akanilaki, kasema, "Mbona unaonekana kuwa na furaha namna hiyo, Billy?"

Nikasema, "Loo, nimekutana na kundi halisi. Jamani, ndilo zuri kuliko yote uliyowahi kuona. Hao watu hawaionei haya dini yao." Na, loo, nilimwambia yote kuhusu jambo hilo. Nami nikasema, "Na tazama hapa, mpenzi, mlolongo mzima wa mialiko. Hao watu!"

Akasema, "Hao si watakatifu wanaojifingirisha, sivyo?"

Nikasema, "Sijui wao ni waviringikaji wa aina gani, bali wanacho kitu nilichohitaji." Mnaona? Nikasema, "Hilo—hilo ni jambo moja ninalojua yakini." Nikasema, "Nilimwona mzee mmoja, umri wa miaka tisini, akiwa kijana tena." Nikasema, "Sijapata kusikia mahubiri kama hayo maishani mwangu. Mbona, sijapata kumwona Mbaptisti akihubiri namna hiyo." Nikasema, "Wanahubiri mpaka wanakosa pumzi, na hukunja magoti wakainama mpaka sakafuni, wakainuka, wakapata pumzi tena. Unaweza kuwasikia umbali wa majengo mawili, bado wanahubiri." Kisha nikasema, "Si—Sijawahi kusikia jambo la namna hiyo maishani mwangu." Basi nikasema, "Wananena kwa lugha isiyojulikana, na yule mwingine anafasiri. Kamwe sijawahi

kusikia jambo la namna hiyo maishani mwangu!" Nikasema, "Je! Utaenda pamoja nami?"

Akasema, "Mpenzi, uliponioa, nitaambatana nawe mpaka kifo kitakapotutenganisha." Akasema, "Nitaenda." Akasema, "Sasa, tutawaambia jamaa zetu."

Nami nikasema, "Vema, mwambie mama yako nami nitamwambia mama yangu." Kwa hiyo sisi ... Nikaenda nikamwambia Mama.

Mama akasema, "Vema, hakika, Billy. Chochote Bwana alichokuitia kufanya, nenda ukakifanye."

95 Na kwa hiyo Bibi Brumbach akaniomba niende kwake. Nikaenda. Akasema, "Ni kitu gani hiki unachozungumzia?"

Nami nikasema, "Loo, Bibi Brumbach," nikasema, "ninyi nyote hamjapata kuwaona watu kama hao."

Akasema, "Tulia! Tulia!"

Nikasema, "Naam, mama." Nikasema, "Samahani."

Naye akasema, "Unajua hilo ni kundi la watakatifu wanaojiviringisha?"

Nikasema, "La, mama, sikujua hilo." Nikasema, "Wao—hao hakika ni watu wazuri."

Akasema, "Hata wazo lenyewe! Unadhani unaweza kumkokota binti yangu umpeleke katika upuzi huo!" Kasema, "Dhihaka hii! Hilo si cho chote bali takataka ambazo makanisa mengine yametupa nje." Akasema, "Hakika! Hutampeleka binti yangu mahali kama hapo."

Basi nikasema, "Lakini, unajua, Bibi Brumbach, kwenye kilindi cha moyo wangu naona kwamba Bwana ananitaka nifuatane na hao watu."

Akasema, "Rudi kanisani kwako mpaka watakapoweza kukupatia nyumba ya kasisi, ukaishi kama mtu aliye na busara." Kasema, "Humpelekei binti yangu kule."

Nikasema, "Naam, mama." Nikageuka nikaondoka.

96 Naye Hope akaanza kulia. Akatoka, akasema, "Billy, haidhuru Mama anasema nini, nitakaa pamoja nawe." Ubarikiwe moyo wake!

Nami nikasema, "Loo, hiyo ni sawa, mpenzi."

Nami nikaliachilia tu. Asingelimruhusu bintiye aende na watu kama hao sababu "Haikuwa kitu ila takataka." Na kwa hiyo kwa namna fulani nikaliachilia. Lilikuwa ni kosa baya zaidi nililowahi kufanya maishani mwangu, moja ya yaliyo mabaya sana.

97 Baadaye kidogo, miaka michache baadaye, watoto wakaja. Na siku moja tulikuwa ... Kulitokea mafuriko, mwaka wa 1937. Kulitokea mafuriko. Na ninii yetu ... Nilikuwa kwenye doria wakati ule na nilikuwa ninajaribu kwa uwezo wangu wote kuwaokoa watu kutoka kwenye mafuriko yale, nyumba zikivunjwa-vunjwa na kuanguka. Na mke wangu mimi akashikwa na ugonjwa, naye alikuwa mahututi sana kwa numonia. Nao wakamtoa nje ... Hospitali ya kawaida yenyewe ilijaa sana kiasi kwamba hatukuweza kumweka mle, kwa hiyo tulimpeleka kwa—kwa ya serikali ambako walikuwa na chumba huko. Ndipo waliniita nirudi. Na siku zote niliishi mtoni, nikiwa nahodha halisi wa boti, kwa hiyo nilikuwa ninajaribu kuwachukua watu, kuwaokoa na yale mafuriko. Na halafu ninge ... mmoja ...

98 Wakaniita, kasema, "Kuna nyumba huko kwenye Barabara ya Chestnut, nusura izame. Kuna mama na watoto kadha mle," kasema, "kama unafikiri boti yako, mota yako inaweza kuwafikia." Nikasema, "Vema, nitafanya yote niwezayo."

Na mimi, nikipiga mawimbi hayo. Boma la kuzuia maji lilikwisha bomoka juu kule, na, loo, jamani, ile... yakibubujikia mjini. Nami ningejitahidi niwezavyo, na hatimaye kule chini kuvuka vichocho vya mji na kupita mahali mbalimbali. Nami nikafika pale karibu na mahali ambapo palikuwa na ukuta wa boma la kale, maji yakibubujikia mle. Ndipo nikasikia mtu akipiga mayowe, kisha nikamwona mama fulani amesimama nje barazani. Na kulikuwa na mawimbi makubwa yakipita hivyo. Naam, nilikwenda juu upande *huu*, kadiri nilivyoweza, nikakumbana na mkondo wa maji nikarudi hata upande ule. Nilikuwa nimesimamisha boti yangu nikiwa nimewahi tu kuifungia kwenye nguzo, nguzo ya mlango, nguzo, au nguzo ya baraza. Basi nikaingia ndani mbio nikamnyakua yule mama na kumwingiza mle, na watoto wawili au watatu. Ndipo nikaifungua boti yangu na nikaipeleka hadi...kurudi. Nikaenda hata kule chini kabisa, nikampeleka hadi ufukoni, yapata maili moja na nusu kuvuka mji, mpaka nikamfikisha ufukoni. Na ndipo nilipofika kule, alikuwa amezimia. Na alikuwa ameanza...alikuwa anapiga mayowe, "Mwanangu! Mwanangu!"

99 Naam, nikafikiri kwamba alimaanisha ameacha mtoto yule kule nyumbani. Loo, jamani! Nikarudi tena wakati walipokuwa wanamwangaalia. Na, nikagundua, ilikuwa...au alikuwa akitaka kujua iwapo mtoto wake

alikuweco. Kulikuwa na jamaa mdogo wa kama miaka mitatu, nami nilifikiria alimaanisha mtoto mchanga anayenyonya au kitu fulani.

Na kwa hiyo nikarudi nikafika kule. Na niliposhuka kwenye boti ile nikaingia mle ndani na sikuweza kuona mtoto ye yote mchanga, ndipo ile baraza ikavunjika na nyumba ikazama. Basi nilikimbia mbio, nikakamata kile—kile kipande pale ambacho kilikuwa kinaelesha motaboti yangu, nikaingia katika ile boti nikakivuta hicho na kuifungulia.

100 Basi ikanipeleka kwenye mkondo wa mto mkubwa. Na ilikuwa kama saa tano u nusu za usiku, huku inanyesha mvua ya theluji. Nami nikashika kamba ya kuipiga stati na nikajaribu kuvuta ile mashua, nayo haikuwaka, nikajaribu tena na haikuwaka, nikajaribu tena. Nikaenda mbali zaidi kwenye mkondo ule, nimekaribia sana yale maporomoko. Nami nilikuwa nikijaribu kwa nguvu sana, na nikawaza, "Loo, jamani, huu—huu ndio mwisho wangu! Ndio huu hapa!" Nami ningejaribu kwa nguvu sana. Ndipo nikasema, "Bwana, tafadhali usiniache nife kifo kama hiki," nami ningevuta na kuvuta.

Basi likanijia tena, "Vipi kuhusu kundi lile la takataka ambalo usingeliendea?" Mnaona? A-ha.

101 Nikarudisha mkono wangu kuuweka kwenye mashua, na nikasema, "Mungu, nirehemu mimi. Usiniache niwaache mke wangu na mtoto mchanga namna hii, nao wako nje huko wakiwa wagonjwa! Tafadhali!" Nami nikaendelea tu kuvuta namna hiyo, nayo haikuwaka. Nami niliweza kusikia ile ngurumo chini kule, sababu mimi... Dakika chache tu, na, loo, jamani, huo ungekuwa ndio mwisho. Basi nikasema, "Bwana, iwapo Wewe utanisamehe, ninakuahidi Wewe nitafanya jambo lo lote." Nikapiga magoti ndani ya mashua ile huku mvua ya theluji ikinipiga usoni. Nikasema, "Nitafanya jambo lo lote ambalo Wewe unataka mimi nifanye." Ndipo nikavuta tena, na ikawaka. Basi nikafungulia petroli yote niliyoweza, na hatimaye nikafika ufukoni.

Nami nikarudi kutafuta lori, lori la doria. Nami nikawazia ... Kulikuwa na baadhi yao waliosema, "Aisee, ile hospitali ya serikali imechukuliwa na maji hivi punde." Mke wangu na mtoto mchanga mle ndani, watoto wote wawili.

102 Basi nikaenda mbio kwenye ile ya serikali upesi nilivyoweza, na maji yalikuwa yamefikia kina cha yapata futi kumi na tano kila mahali. Na palikuwa na meja pale, na nikasema, "Meja, nini kimeikumba hospitali?"

Kasema, "Sasa, usiwe na wasiwasi. Una mtu yeyote mle ndani?"

Nikasema, "Naam, m—mke mgonjwa na watoto wawili wachanga."

Yeye alisema, "Wote walitoka." Kasema, "Wako kwenye gari la mizigo na wameelekea Charlestown."

Nikakimbia, nikaigia katika mashua yangu na...au nikaingia katika motokaa yangu, na mashua yangu nyuma yake, nikakimbilia kule kuninii... Ndipo basi vijito vilikwisha pungua vikawa na upana wa maili mbili na nusu au tatu. Na usiku kucha nilijaribu kuninii ... Baadhi yao walisema, "Gari, gari la mizigo, lilichukuliwa na maji huko kwenye daraja."

Naam, nikajikuta nimeachwa peke yangu kwenye kisiwa kidogo, nikakaa pale siku tatu. Nilikuwa na muda wa kutosha kufikiria kama kundi Hilo lilikuwa ni takataka au la. Nikipigapiga tu, "Mke wangu yuko wapi?"

103 Hatimaye nilipompata, mnamo siku chache baada ya kutoka kule na kuvuka, alikuwa huko mbali Columbus, Indiana, katika Jumba la Mikutano la Kibatisti ambako wamefanya na—namna ya hospitali, vyumba vya wagonjwa kwenye vitanda vidogo vya serikali. Nami nikamkimbilia kwa nguvu niwezavyo, nikijaribu kupata mahali alipokuwa, nikipaza sauti, "Hope! Hope! Hope!" Ndipo niliangalia, huyo hapo amelala kwenye machela, pia ameugua kifua kikuu.

Akainua mkono wake mdogo, na kusema, "Billy."

Nami nikamkimbilia, nikasema, "Hope, mpenzi."

Akasema, "Ninaonekana mbaya sana, sivyo?"

Nikasema, "La, mpenzi, unaonekana sawa."

104 Kwa yapata miezi sita tulifanya kazi kwa bidii sana, kujaribu kuyaokoa maisha yake, lakini aliendelea kudhoofika.

Siku moja nilikuwa kwenye doria na nilikuwa nimeifungulia redio yangu, nami nilifikiria nilisikia wakisema, wakiita kwenye redio, kasema, "Kwa William Branham, unatakiwa hospitalini mara moja, mkeo yuafa." Nikarudi hospitalini haraka nilivyoweza, nikawasha kimulimuli na kupiga king'ora nikaondoka. Ndipo ni—nikafika hospitali nikasimama, nikaingia ndani haraka. Nikashuka nikaenda ho—hospitalini, nikamwona maskini rafiki yangu ambaye tulivua samaki pamoja, tulicheza pamoja kama wavulana, Sam Adair.

Daktari Sam Adair, yeye ndiye ambaye lile ono lilikuja kwa ajili yake si muda mrefu uliopita na kumwambia kuhusu ile hospitali. Naye alisema, kama mtu ye yote alitilia shaka lile ono, hebu ampigie simu bila malipo kama wanataka kujua kama ilikuwa kweli au la.

105 Na kwa hiyo basi huyu hapa anatokea namna hiyo, naye alikuwa na kofia yake mkononi mwake. Aliniangalia na akaanza kulia tu. Nami nikamkimbilia, nikamkumbatia. Akanikumbatia, akasema, "Billy, anaaga dunia." Akasema, "Ninasikitika. Nimetenda yote nilivyoweza kutenda, nimeemletea wataalam maalum na kila kitu."

Nikasema, "Sam, hakika haagi dunia!"

Kasema, "Naam, anaondoka."

Naye akasema, "Usiingie kule, Bill."

Nami nikasema, "Sina budi kuingia, Sam."

Naye akasema, "Usifanye hivyo. Usiingie, tafadhali usifanye hivyo."

Nikasema, "Tafadhali niruhusu niingie."

Kasema, "Nitaenda pamoja nawe."

Nikasema, "La, wewe kaa hapa nje. Ninataka kukaa naye katika dakika zake za mwisho."

Kasema, "Amepoteza fahamu."

106 Nikaingia chumbani. Naye nesi alikuwa ameketi pale, naye alikuwa analia maana yeye na Hope walikuwa wakisoma pamoja. Na kwa hiyo nikamtazama, naye akaanza kulia, akainua mkono wake. Ndipo akaanza kuondoka.

Ndipo nikaangalia, na kumtikisa. Huyu hapo, alikwisha pungua toka kama ratili mia moja na ishirini, hadi yapata sitini. Nami ni—nikamtikisa. Na kama nitaishi nifikie umri wa miaka mia, sitasahau kilichotukia. Aligeuka, na yale macho makubwa mno na mazuri yakanitazama. Alitabasamu. Akasema, "Kwa nini uliniita nirudi, Billy?"

Nikasema, "Mpenzi, hivi punde nimepata fedha tasilimu ..."

107 Ilinibidi kufanya kazi. Tulikuwa na deni kubwa sana na mamia ya dola za bili ya daktari, na hatuna kitu cha kulipia. Nami ilinibidi tu kufanya kazi. Nami nilienda kumtazama mara mbili au tatu kwa siku, na kila usiku, na hapo alipokuwa katika hali ile.

Nikasema, "Unamaanisha nini, 'Kukuita' urudi?"

Akasema, "Bill, umehubiri habari Zake, umenena habari Zake, bali hujui ni kitu gani."

Nikasema, "Unazungumzia nini?"

Akasema, "Mbinguni." Akasema, "Angalia," akasema, "nilikuwa ninasindikizwa Nyumbani na watu fulani, wanaume au wanawake au wo wote wale. Walikuwa wamevaa nguo nyeupe." Naye akasema, "Nilikuwa na raha na amani." Kasema, "Ndege wakubwa wazuri wakiruka kutoka mti hadi mti." Akasema, "Usidhani nimerukwa na akili." Akasema, "Billy, nitakwambia kosa letu." Akasema, "Keti chini." Sikuketi; nilipiga magoti, nikashika mkono wake. Akasema, "Unajua kosa letu liko wapi?"

Nami nikasema, "Naam, mpenzi, ninajua."

Akasema, "Hatukupaswa kamwe kumsikiliza Mama. Hao watu walikuwa sahihi."

Nami nikasema, "Ninajua jambo hilo."

Akasema, "Niahidi jambo hili, ya kwamba utawaendea watu hao," kasema, "kwa sababu wako sahihi." Naye akasema, "Walee watoto wangu namna hiyo." Nami ... Akasema, "Nataka kukwambia jambo fulani." Akasema, "Ninakufa, lakini" kasema "ni ... Si—siogopi kwenda." Kasema, "Ni—ni kuzuri." Akasema, "Ila tu, nachukia kukuacha, Bill. Nami najua una watoto hawa wawili wachanga wa kulea." Akasema, "Niahidi kwamba—kwamba hutakaa bila mke na kuwacha watoto wangu wachukuliwe huku na huko." Hilo lilikuwa ni jambo la busara kwa mama mwenye umri wa miaka ishirini na moja.

Nami nikasema, "Siwezi kuahidi jambo hilo, Hope."

Akasema, "Tafadhali niahidi." Kasema, "Nataka kukuambia jambo moja." Kasema, "Unakumbuka ile bunduki?" Ninapenda bunduki sana. Basi akasema, "Ulitaka kununua raifoo ile siku ile nawe hukuwa na fedha za kutosha kwa malipo ya kwanza."

Nikasema, "Naam."

Akasema, "Nimekuwa nikiweka fedha yangu, hela zangu, kujaribu kutoa malipo ya kwanza ya raifoo ile kwa ajili yako." Akasema, "Sasa, haya yatakapomalizika nawe urudi nyumbani, angalia kwenye kile kitanda cha kukunja...au kitanda cha kukunja, chini ya kipande kile cha karatasi huko juu, nawe utazipata hizo fedha humo." Akasema, "Niahidi kwamba utanunua bunduki hiyo."

Hujui jinsi nilivyojihisi wakati nilipoona ile dola na senti sabini na tano (katika hela) zimewekwa mle. Nikanunua ile bunduki.

108 Naye akasema, "Unakumbuka hapo ulipokuwa ukishuka kwenda mjini kuninunulia jozi ya soksi ndefu, nasi tulikuwa tunakwenda Fort Wayne?"

Nikasema, "Naam."

Nilikuwa nimerudi toka kuvua samaki, naye akasema... Ilitubidi kwenda Fort Wayne, ilinipasa kuhubiri usiku ule. Naye akasema, "Unajua, nilikwambia, 'Kuna aina mbili tofauti.'" Moja iitwayo "chiffon." Na ile nyingine ni nini, rayon? Hiyo ni kweli? Rayon na chiffon. Vema, lo lote lile, chiffon ndiyo iliyokuwa nzuri kuliko zote. Hiyo ni kweli? Ndipo akasema, "Sasa, hebu ninunulie chiffon, mtindo kamili." Unajua kitu kile ambacho kina kitu kidogo nyuma ya soksi sehemu ndefu, juu? Nami sikujua kitu kuhusu nguo za wanawake, kwa hiyo ni...

Nami nilikuwa nikishuka kwenda barabarani na kusema, "Chiffon, chiffon, chiffon, chiffon," nikijaribu kuendelea kuwazia, "chiffon, chiffon, chiffon."

Mtu fulani akasema, "Habari zako, Billy!"

Nikasema, "Loo, sijambo, sijambo." "Chiffon, chiffon, chiffon, chiffon, chiffon."

Basi nikafika pembeni nikakutana na Bw. Spon. Akasema, "Habari zako, Billy, unajua wanadonoa sasa upande ule wa gati?"

Nikasema, "Bila shaka, hilo ni kweli?"

"Naam."

Nikawaza sasa, nilipomwacha, "Kitu kile kilikuwa ni nini?" Nimekisahau.

109 Kwa hiyo Thelma Ford, msichana niliyemjua, alifanya kazi kwenye duka la rejareja. Basi nilijua waliuza soksi ndefu za wanawake pale, kwa hiyo nilikwenda huko. Nikasema, "Halo, Thelma."

Naye akasema, "Halo, Billy. U hali gani? Habari za Hope?"

Basi nikasema, "Mzima." Nikasema, "Thelma, nataka jozi ya soksi kwa ajili ya Hope."

Akasema, "Hope hahitaji soksi."

Nikasema, "Ndiyo, mama, hakika anazihitaji."

Kasema, "Unamaanisha soksi ndefu."

"Loo, hakika," nikasema, "ndizo hizo." Nikawaza, "A-ha, tayari nilionesha ujinga wangu."

Naye akasema, "Anataka aina gani?"

Nikawaza, "Lo-enhee!" Nikasema, "Una aina gani?"

Akasema, "Vema, tuna rayon."

110 Sikujua tofauti yake. Rayon, chiffon, yote inasikika sawa. Nikasema, "Nataka hiyo." Akasema ... Nikasema, "Nifungie jozi yake, staili kamili." Na yeye... Nilikosea hilo. Ni kitu gani? Mtindo kamili. "Mtindo kamili." Na kwa hiyo nilisema, "Nifungie jozi ya hizo."

Naye aliponipa, zilikuwa kama senti thelathini tu, senti ishirini au senti thelathini, kama nusu ya bei. Vema, nikasema, "Nipe jozi mbili." Mnaona?

111 Nami nikarudi nyumbani, na nikasema, "Unajua, mpenzi, ninyi wanawake mnazunguka mji mzima kubishana bei ya bidhaa." Unajua jinsi unavyopenda kuwika. Ndipo nikasema, "Lakini hapa, angalia hapa, nimenunua jozi mbili kwa bei ambayo mnanunulia jozi moja. Mnaona?" Nikasema, "Loo, huo huo ni uwezo wangu binafsi." Unaona, nikasema—nikasema, "Unajua, Thelma, aliniuzia hizi." Nikasema, "Pengine ameniachia nizichukue kwa nusu ya bei yake."

Akasema, "Ulipata chiffon?"

Nikasema, "Naam, mama." Yote yanasikika ni mambo kwangu, sikujua kulikuwa na tofauti yo yote.

112 Naye akaniambia, akasema, "Billy." Nilishangaa wakati alipofika Fort Wayne, ilibidi anunue jozi nyingine ya soksi ndefu. Alisema, "Nilimpa mama yako hizo," kasema, "ni za wanawake wazee." Kasema, "Ninasikitika nilitenda jambo hilo."

Ndipo nikasema, "Hilo ni sawa, mpenzi."

Naye akasema, "Sasa, usi—usiishi peke yako." Naye akasema ... Hakujuua ambacho kingetukia katika masaa machache tokea hapo. Nami nikashika mikono yake mizuri wakati Malaika wa Mungu walipomchukua.

113 Nilienda nyumbani. Sikujua la kufanya. Nililala pale usiku na nikasikia ... Nafikiri ilikuwa panya mdogo, alikuwa katika nondo za lile jiko kuukuu ambamo tuliweka makaratasi. Basi nikafunga mlango kwa mguu wangu, na hapo palining'inia nguo yake ya kimondo hapo nyuma, (naye amelala chini kule kwenye kile chumba cha maiti). Na katika muda mfupi tu mtu fulani akanipigia simu, akasema, "Billy!" Na ilikuwa ni Ndugu Frank Broy. Akasema, "Mtoto wako mchanga yuafa."

Nikasema, "Mtoto wangu mchanga?"

Kasema, "Naam, Sharon Rose." Kasema, "Dakt yuko juu'Anae sasa, kisha akasema, 'Ana homa ya uti wa mgongo, aliambukizwa na mama yake.'" Kisha akasema, "Anakufa."

114 Nikaingia kwenye gari, nikapanda kwenda kule. Huyu hapo, kitoto kipenzi. Nao wakamkimbiza hospitalini.

Nilitoka kwenda kumwona. Sam akaja na kusema, "Billy, usiingie kwenye chumba hicho, huna budi kumfikiria Billy Paul." Kasema, "Anakufa."

Nikasema "Dakt, ya—yanipasa kumwona mtoto wangu mchanga."

Akasema, "La, huwezi kuingia." Kasema, "Ana homa ya uti wa mgongo, Billy, nawe ungemwambukiza Billy Paul."

115 Basi nikangojea mpaka alipotoka nje. Nisingeweza kuvumilia kumwona akifa, na mama yake amelala chini kule kwenye chumba cha maiti. Nawaambia, njia ya mkosaji ni ngumu. Basi ni—nikaenda, nikapenyeza mlangoni, basi Sam alipotoka nje pamoja na mwuguzi, nilienda kwenye orofa ya chini. Ni hospitali ndogo sana. Alikuwa mahali palipotengwa, na inzi walikuwa kwenye macho yake. Nao walikuwa na ninino ndogo...tunayoita "kizuizi cha mbu," au chandalua kidogo kwenye macho yake. Naye angeninino...na mshtuko mdogo, mguu wake mdogo mnene ulikuwa unasogea juu na chini namna hiyo, na mikono yake midogo, na mshtuko ule. Nami nikamwangukia, na yeye alikuwa mkubwa vya kutosha kuwa mrembo, kama umri wa miezi minane.

116 Na mama yake alizoea kumweka nje kule na gari lake lenye magurudumu matatu, wajua, uwanjani, nilipokuwa nikija. Na ningepiga honi, naye angefanya, guu—guu, guu—guu, akininyoshea mikono, mnajua.

Na hapo alilala mpenzi wangu, anakufa. Nikamtazama pale chini, nami nikasema, "Sharry, unamjua Baba? Unamjua Baba, Sharry?" Na wakati alipoangalia ... Alikuwa anateseka sana mpaka moja la hayo macho madogo ya samawati lilikengeza. Karibu jambo hilo linivunje moyo kabisa.

Nikapiga magoti, nikasema, "Bwana, nimefanya nini? Sikuhubiri Injili kwenye kila sehemu mitaani? Nimefanya kila nijuacho kufanya. Usinipatilize kwa jambo hilo. Sikuwaita kamwe hao watu 'takataka.'" Bibi huyo ndiye aliyewaita hao watu 'takataka.'" Nikasema, "Ninasikitika yote hayo yalitukia. Nisamehe. Usi—usimchukue mtoto wangu mchanga." Na wakati nilikuwa ninaomba, ilionekana kama kitu cheusi...kama shuka au nguo ilitelemka. Nilijua alikuwa amenikatalia.

117 Sasa, huo ulikuwa ndio wakati mgumu zaidi na wa hatari sana maishani mwangu. Niliposimama na kumtazama, nami nikawazia ... Shetani akaninong'onezea, "Vema, wataka kusema jinsi ulivyohubiri kwa bidii, na jinsi ulivyoishi, na sasa inapofika kwa mtoto wako binafsi aliye mchanga, Yeye atakukatalia?"

Nami nikasema, "Hiyo ni kweli. Kama hawezi kumwoko mtoto wangu mchanga, basi siwezi ..." Nikanyamaza. Si—sikujua tu la kufanya. Halafu basi nikasema hivi, nikasema, "Bwana, Wewe ulinipa huyu na Wewe umemchukua, na libarikiwe Jina la Bwana! Hata kama utanichukua mimi, bado nitakupenda Wewe."

Ndipo nikaweka mkono wangu juu yake, nikasema, "Ubarikiwe, kipenzi. Baba alitaka kukulea, kwa moyo wangu wote nilitaka kukulea, na kukulea ukampende Bwana. Lakini Malaika wanakuja kukuchukua, kipenzi. Baba atachukua mwili wako mdogo aupeleke kule chini akauweke mikononi mwa Mama. Nitakuzika pamoja naye. Siku moja Baba atakutana nawe, wewe ngoja tu kule juu pamoja na Mama."

118 Mama yake alipokuwa anakufa, alisema, maneno ya mwisho aliyosema, alisema, "Bill, usiache

kuhubiri.”

Nikasema, “Nita- ...” Akasema ... Nikasema, “Kama nitakuwa ninahubiri wakati Yeye ajapo, nitawachukua watoto tukamlaki. Kama sitafanya hivyo, nitazikwa karibu na wewe. Nawe nenda upande wa kuume wa lile lango kuu, na hapo utakapowaona wote wakiingia, simama pale uanze kupiga kelele, 'Bill! Bill! Bill! kwa nguvu uwezavyo. Nitakutana nawe kule.” Nikambusu kwaheri. Niko kwenye uwanja wa vita leo. Hiyo imekuwa karibu miaka ishirini iliyopita. Nimepeana miadi na mke wangu, nitakutana naye.

119 Basi nikamchukua yule mtoto mchanga, na alipokufa, nikamweka kwenye mikono ya mama yake, nasi tukamchukua kwenye makaburi. Ndipo nilisimama pale kumsikia Ndugu Smith, mhubiri wa Kimethodisti ambaye aliongoza ibada ya mazishi. (Nami nikawaza, “Moyo kwa moyo.”) Huyo hapo akaenda.

Si muda mrefu baada ya jambo hilo, nilienda huko na Billy asubuhi moja. Yeye alikuwa ni jamaa mdogo tu. Alikuwa ...

Hiyo ndiyo sababu haniachi nami simwachi, ilibidi niwe vyote viwili Baba na Mama (wote wawili) kwake. Ningechukua chupa yake ndogo. Hatukumudu kuwa na moto usiku kuchemsha maziwa, yake, na ningeiweka chini ya mgongo wangu namna hii na kuyapasha moto kwa joto la mwili wangu.

Tumeshikana pamoja kama marafiki wazuri sana, na siku moja nikiondoka uwanjani nataka kumkabithi Neno, na kusema, “Endelea, Billy. Dumu nalo.” Baadhi ya watu wanashangaa kwa nini niko pamoja naye wakati wote. Siwezi kumwacha. Yeye hata ameo, lakini bado ninakumbuka alioniambia, “Usimwache.” Nasi tulishikamana kama marafiki.

120 Nakumbuka nikitembea mjini, chupa kwapani mwangu, angeanza kulia. Usiku mmoja alikuwa ... alikuwa anatembea nje uwani ambako tu... (Wakati alipokuwa anajiandaa kumzaa, yeye alikuwa anasongwa moyo, nami ... msichana tu, mnajua.) Nami ningetembea huku na kule toka kwenye ule mwaloni kwenye uwanja wa nyuma. Naye alikuwa anamlilia Mama yake, nami sina Mama wa kumpelekea. Basi ningembeba, ningesema, “Loo, mpenzi.” Nikasema ...

Akasema, “Baba, mama yangu yuko wapi? Je, wewe ulimweka katika ardhi?”

Nikasema, “La, mpenzi. Yeye ni mzima, yuko juu Mbinguni.”

121 Naye akasema jambo fulani pale, nusura liniue alasiri moja. Alikuwa analia, ilikuwa karibu usiku, nami nilikuwa nimembeba mgongoni mwangu namna hii, nikimbeba begani mwangu na kumpigapiga *hivi*. Naye akasema, “Baba, tafadhali nenda ukamchukue Mama umlete hapa.”

Nami nikasema, “Mpenzi, siwezi kumpata Mama. Yesu ...”

Kasema, “Vema, mwambie Yesu aniletee mama yangu. Ninamtaka.”

Nami nikasema, “Vema, mpenzi, mimi...mimi na wewe tutamwona siku moja.”

Ndipo akanyamaza, akasema, “Baba!”

Nami nikasema, “Naam?”

Kasema, “Nilimwona Mama kule juu kwenye hilo wingu.”

Jamani, karibu nizimie! Nikawaza, “Jamani! 'Nilimwona Mama kule juu kwenye lile wingu.'” Karibu nizimie tu. Nikamkumbatia jamaa mdogo huyo kwenye kifua changu *hivi*, na kuinamisha kichwa changu chini, nikaingia ndani.

122 Siku zikapita. Nisingeweza kusahau jambo hilo. Nilijaribu kufanya kazi. Singerudi nyumbani, haikuwa ni nyumbani tena. Nami nilitaka kukaa. Hatukuwa na kitu ila tu fanicha ile kuukuu na iliyochakaa, lakini ilikuwa ni kitu ambacho mimi na yeye tulifurahia pamoja. Ilikuwa ni nyumbani.

Nami ninakumbuka siku moja nilikuwa nikijaribu kufanya kazi katika utumishi wa umma. Nilikuwa nimekwenda kutengeneza waya ndogo kuukuu za umeme, zilikuwa zinaning'inia, ilikuwa asubuhi na mapema. Nami nikapanda hadi hapa zinapopitana. (Nami sikuweza kumsahau mtoto yule. Nilivumilia kumwona mke wangu akiaga dunia, lakini yule mtoto mchanga akiaga dunia, kitoto kichanga tu.) Nami nilikuwa kule, na nilikuwa nikiimba, “Kwenye kilima cha mbali, palisimama Msalaba wa kale ulioparua.” Na zile waya ndogo za umeme zilishuka chini kwenye transfoma na kutoka katika (unajua) kwenye zile kubwa. Nami nilikuwa ninaning'inia kule juu yake. Na ikatukia kwamba nilitazama, huku jua linachomoza nyuma yangu. Na pale, mikono yangu imenyoosha huku ishara ya Msalaba ule ka—kando ya kilima. Nikawaza, “Ndiyo, dhambi zangu ndizo zilizomweka Yeye pale.”

123 Nikasema, “Sharon, mpenzi, Baba yako anataka sana kukuona, mpenzi. Jinsi ningependa kukushika mikononi mwangu tena, maskini kipenzi changu.” Nikachanganyikiwa kabisa... Imepita majuma kadhaa. Nikavua glovu zangu za plastiki. Kuna voti elfu mbili na mia tatu zinatiririka karibu kabisa nami. Nikavua

glavu zangu za plastiki. Nikasema, "Mungu, ninachukia kutenda jambo hili. Mimi ni mwoga." "Lakini, Sherry, Baba anakuja kukuona pamoja na Mama mnamo dakika chache tu." Nikaanza kuvua glavu zangu, kuweka mkono wangu kwenye zile voti elfu mbili na mia tatu. Ingevunja... Mbona, hata usingekuwa na damu iliyobakia ndani yako. Na kwa hiyo ni—ni—nikaanza kuitoa hiyo glavu, na kitu fulani kikatendeka. Nilipopata kujirudia, nilikuwa nimekaa chini ardhini na mikono yangu juu namna hii, kwenye uso wangu, nikilia. Ilikuwa neema ya Mungu, la sivyo singekuwa ninaendesha ibada ya kuponya hapa, nina hakika na jambo hilo. Ilikuwa ni Yeye akilinda kipawa Chake, si mimi.

124 Nikaanza kwenda nyumbani. Nikaacha, nikaweka vyombo vyangu. Nikarudi, nikasema, "Ninakwenda nyumbani."

Nikaanza kuzunguka nyumba, kisha nikachukua barua nyumbani, ilikuwa baridi kidogo, basi nikaingia ndani. Tulikuwa na chumba kimoja kidogo, nilikuwa ninalala kwenye kitanda kidogo pale, na ukungu ukija, na jiko hilo kuukuu. Nikachukua zile barua na nikazisoma, na jambo la kwanza pale lilikuwa hela zake chache za akiba kwa ajili ya Krismasi, senti themanini, "Bi Sharon Rose Branham." Hilo hapo, limerudi tena.

125 Nimekuwa mlinzi wa wanyama pori. Nikaunyosha mkono mle ndani nikachukua bunduki yangu, bastola, kutoka kwenye mfuko wake. Nikasema, "Bwana, si—siwezi kuendelea hivi tena, ni—ninakufa. Mimi ni—ninaateswa sana." Nikafungua usalama wa bunduki, nikailenga kichwani, huku nimepiga magoti pale kwenye kitanda kile katika chumba hicho chenye giza. Nikasema, "Baba yetu uliye Mbinguni, Jina Lako litukuzwe. Ufalme Wako na uje, mapenzi Yako yatimizwe," ndipo nilipojaribu, nikafinya mtambo wa kufyatulia kwa nguvu kadiri nilivyoweza, nikasema, "duniani kama huko Mbinguni. Utupe leo chakula chetu cha kila siku." Nayo haingefyatuka!

Basi nikawaza, "Ee Mungu, Wewe unanirarua vipande-vipande? Nimefanya nini? Hata hutaniruhusu nife." Nami nikaitupa bunduki ile chini, nayo ikafyatukia chumbani. Ndipo nikasema, "Mungu, kwa nini nisife na kuachana na jambo hilo? Siwezi kuendelea mbele zaidi. Huna budi kunitendea jambo fulani." Nami nikaanguka chini na kuanza kulia kwenye kitanda changu kidogo na kichafu cha kale pale.

Na sina budi nililala. Sijui kama nilikuwa nimelala au nini kilitukia.

Sikuzote nimetamani kwenda Magharibi. Daima nimetaka moja ya hizo kofia. Baba yangu aliwafundisha farasi katika siku za ujana wake, nami nilitaka moja ya hizo kofia. Na Ndugu Demos Shakarian alininunulia moja jana, ya kwanza niliyopata kuwa nayo (niliyowahi kuwa nayo) ya namna hiyo, moja ya hizo kofia za magharibi.

126 Nami nikawaza ninashuka nikipitia mbugani, nikiimba wimbo ule, "Kuna gurudumu la gari la farasi lililovunjika, kwenye ranchi, 'Linanzwa.'" Basi nilipoendelea, nikaona gari kubwa la farasi lenye turubai, kama gari la kale la mbugani, huku gurudumu lake limevunjika. Bila shaka, hiyo iliwakilisha familia yangu iliyovunjika. Nami nilipokaribia, nikaangalia, na hapo palisimama m—msichana mdogo na mrembo sana, yapata umri wa miaka ishirini, nywele nyeupe zinazoning'inia chini na macho ya samawati, amevaa nguo nyeupe. Nikamwangalia, nikasema, "U hali gani?" Nikaendelea.

Akasema, "Sijambo, Baba."

Nami nikageuka nyuma, nikasema, "Baba?" "Mbona," nikasema, "vipi, Binti, unaweza...ninawezaje kuwa baba yako na huku tuna umri mmoja?"

Akasema, "Baba, hujui kabisa uko wapi." Nami nikasema, "Unamaanisha nini?"

Akasema, "Hapa ni Mbinguni." Kasema, "Duniani nilikuwa mtoto wako Sharon."

"Mbona," nikasema, "mpenzi, ulikuwa mtoto mchanga tu."

Kasema, "Baba, watoto wachanga si watoto wachanga humu, wao hawapatikani na mauti. Hawazeeki wala kukua kamwe."

Nami nikasema, "Vema, Sharon, mpenzi, u—u kijana mwanamke mrembo."

Akasema, "Mama anakungojea."

Nami nikasema, "Wapi?"

Akasema, "Huko juu kwenye nyumba yako mpya."

Nami nikasema, "Nyumba mpya?" Wabranham ni watu wa kutangatanga, hawana makao, wao tu... Basi nikasema, "Vema, sijawahi kuwa na nyumba, mpenzi."

Akasema, "Lakini una mmoja hapa, Baba." Simaanishi kuwa mtoto mchanga, bali ni halisi sana kwangu. [Ndugu Branham analia — Mh.] Ninapoanza kuwazia jambo hilo, yote yanarudi tena. Kasema,

“Una moja hapa, Baba.” Ninajua nina moja kule, siku moja nitaiendea. Akasema, “Yuko wapi Billy Paul, ndugu yangu?”

Ndipo nikasema, “Vema, nilimwacha kwa Bibi Broy, dakika chache tu zilizopita.”

Kasema, “Mama anataka kukuona.”

127 Basi nikageuka na kutazama, na kulikuwa na majumba makubwa mno ya kifalme, na Utukufu wa Mungu ukija kuyazunguka. Kisha nikasikia kwaya ya Malaika ikiimba, “Makao yangu, Makao mazuri.” Nikaanza kupanda vipandio nikipiga hatua ndefu, nikikimbia mbio nilivyoweza. Na nilipofika mlangoni, huyo hapo amesimama, amevaa vazi jeupe, zile nywele nyeusi na ndefu, zinazofunika mgongo wake. Akainua mikono yake, kama alivyofanya sikuzote nilipokuja nyumbani nimechoka kutoka kazini au kitu fulani. Nikamshika mikono, nikasema, “Mpenzi, nimemwona Sharon chini kule.” Nikasema, “Amekuwa msichana mrembo, sivyo?”

Akasema, “Naam, Bill.” Akasema, “Bill.” Akanikumbatia, (naye akasema) kwenye mabega yangu, akaanza kunipigapiga akasema, “Acha kunifadhaikia mimi na Sharon.”

Nikasema, “Mpenzi, siwezi kujizuia.”

Akasema, “Sasa mimi na Sharon tuna hali nzuri kuliko wewe.” Kisha kasema, “Usitufadhaikie sisi tena. Utaniahidi?”

Ndipo nikasema, “Hope,” nikasema, “nimekuwa na ukiwa sana kwa ajili yako wewe na Sharon, na Billy anakulilia wewe wakati wote.” Nikasema, “Sijui nifanyeje naye.”

Basi akasema, “Mambo yatakwenda sawa, Bill.” Akasema, “Niahidi tu hutafadhaika tena.” Naye akasema, “Tafadhali keti.” Basi nikaangalia pande zote na palikuwa na kiti maarufu kikubwa mno.

128 Nami ninakumbuka nilijaribu kununua kiti. Sasa, katika kufunga. Nilijaribu kununua kiti wakati mmoja. Tulikuwa tu na hivyo viti vikuukuu—viti vya kawaida vyenye vikatio vya mbao kwa ile seti ya kifunguakinywa. Ilibidi tuvitumie, ndivyo viti pekee tulivyokuwa navyo. Na tungeweza kununua moja ya viti hivi ambavyo unavikunjua viegemee nyuma, kama... Ninasahau ni kiti aina gani cha kustarehe. Nacho kiligharimu dola kumi na saba, na ungeweza kulipa dola tatu kwanza na dola moja kwa juma. Nasi tukapata kimoja. Na, loo, wakati ningekuja ... Ningefanya kazi mchana kutwa, na kuhubiri mpaka usiku wa manane barabarani na po pote nilipoweza kuhubiri.

Na—na siku moja nikachelewa kulipa malipo yangu. Hatungeweza kulipa, basi ikawa hivyo siku baada ya siku, hatimaye siku moja wakaja wakachukua kiti changu wakaenda nacho. Usiku huo, sitasahau kamwe, aliniokea sambusa ya matunda. Maskini mama huyo, yeye—yeye—yeye alijua ningekata tamaa. Na baada ya chakula cha jioni nikasema, “Kitu gani kinakufanya uwe mwema namna hiyo usiku wa leo, mpenzi?”

Naye akasema, “Aisee, niliwaleta vijana majirani hapa kukuchimbulia wadudu wa vyambo vya kuvulia samaki. Si ni afadhali twende chini mtoni tukavue kwa muda kidogo?”

Nami nikasema, “Naam, lakini ...”

129 Ndipo akaanza kulia. Nilijua kuna jambo limeenda kombo. Nilikuwa na fununu sababu walikuwa tayari wameisha nipelekea notisi wangukuja kukitwaa. Nasi tusingeweza kufanya malipo hayo ya dola kwa juma moja. Hatungeweza, hatuku ... tusingeweza kumudu. Alinikumbatia, na nikaenda mlangoni na kiti changu kilikuwa kimechukuliwa.

Akaniambia kule Juu, akasema, “Unakumbuka kile kiti, Bill?”

Nami nikasema, “Naam, mpenzi, nakumbuka.”

Kasema, “Hicho ndicho ulichokuwa unafikiria, sivyo?”

“Naam.”

Kasema, “Vema, hawatakichukua hiki, hiki kimelipiwa.” Akasema, “Keti chini kidogo, nataka kuzungumza nawe.”

Nami nikasema, “Mpenzi, sielewi jambo hili.”

Naye kasema, “Niahidi, Billy, niahidi kwamba hutafadhaika tena. Unarudi sasa.” Kisha akasema, “Niahidi hutafadhaika.”

Nami nikasema, “Siwezi kufanya hivyo, Hope.”

130 Mara nikapata jirudia, kulikuwa giza chumbani. Nikaangalia kila upande, huku ninausia mkono wake

umenikumbatia. Nikasema, "Hope, umo humu chumbani?"

Akaanza kunipigapiga. Akasema, "Utanipa ahadi hiyo, Bill? Niahidi hutaoa...hutafadhaika tena."

Nikasema, "Ninakuahidi."

Na kisha aliponipigapiga mara mbili tatu, akaondoka. Nikaruka juu na kuwasha taa, nikatazama kila mahali, aliisha kwenda. Bali alitoka tu mle chumbani. Hajaondoka, angali anaishi. Alikuwa ni Mkristo.

131 Mimi na Billy tulikwenda kwenye kaburi hapa wakati fulani uliopita, tukibeba maua machache kwa ajili ya mama yake na dada yake, kwenye asubuhi ya Pasaka, nasi tukasimama. Mtoto huyo akaanza kulia, akasema, "Baba, mama yangu yuko chini kule."

Nikasema, "La, mpenzi. La, yeye hayuko chini kule. Dada hayuko huko chini. Tuna kaburi lililofunikwa hapa, bali huko mbali ng'ambo ya bahari kuna kaburi lililo wazi ambamo Yesu alifufuka. Na siku moja Yeye atakuja, Yeye atamleta dada na mama pamoja Naye."

Niko kwenye uwanja wa vita leo, marafiki. Si—siwezi kusema lolote zaidi. Mimi ... [Ndugu Branham analia — Mh.] Mungu akubariki. Hebu na tuinamishe vichwa vyetu kwa dakika moja.

132 Ee Bwana! Mara nyingi, Bwana, nina hakika watu hawaelewi, wanapofikiria mambo haya huja kwa urahisi. Bali kuna siku kuu ijayo Yesu atakapokuja na huzuni hizi zote zitafutiliwa mbali. Naomba, Baba wa Mbinguni, kwamba Wewe utatusaidia kujiandaa.

Na ahadi ile ya mwisho, nilipombusu kwenye shavu asubuhi ile, kwamba ningekutana naye huko siku ile. Naamini atakuwa amesimama kwenye ile nguzo, akiliita jina langu kwa sauti kubwa. Nimeishi mwaminifu kwa ahadi ile tangu wakati huo, Bwana, ulimwenguni kote, katika sehemu za kila aina, nikijaribu kuileta Injili. Ninazeeka sasa na kuchoka, nimechakaa sana. Siku moja hivi punde nitafunga Biblia hii kwa mara ya mwisho. Basi, Mungu, niweke mwaminifu kwa ahadi ile. Nizungushie neema Yako, Bwana. Jalia nisyatazame mambo ya maisha haya, niishi kwa ajili ya mambo yaliyo kule ng'ambo. Nisaidie kuwa mwaminifu. Siombi maisha yaliyo rahisi, la, Bwana, na huku Kristo wangu alikufa matesoni. Na hao wengine wote walikufa namna hiyo. Siombi jambo lo lote rahisi. Hebu tu niwe mwaminifu, Bwana, mkweli. Hebu watu wanipende ili niweze kuwaongoza Kwako. Ndipo siku moja wakati yote yameisha nasi tumekusanyika pamoja chini ya miti isiyokauka, nataka kumshika mkono na kumpandisha juu, kuwaonesha watu wa Angelus Temple na wengine wote. Utakuwa basi wakati wa furaha kuu.

Ninaomba ya kwamba rehema Zako ziwe juu ya kila mmoja wetu hapa. Na wale walio hapa, Bwana, huenda hata wasikujue Wewe. Na pengine baadhi ya maskini wapenzi wao wako kule ng'ambo ya bahari. Iwapo hawajatimiza ahadi yao, hebu na wafanye hivyo sasa, Bwana.

133 Huku vichwa vyetu vimeinamishwa, sijui katika jengo hili kubwa mno la mikutano adhuhuri hii, ni wangapi wenu wanasema "Ndugu Branham, ninataka kukutana na wapenzi wangu, pia. Ni—ni—ninao baadhi ya wapenzi wangu kule ng'ambo ya pili ya mto."? Pengine uliahidi kwamba utakutana nao, pengine ulipomwambia mama "kwa heri" juu kule kaburini siku ile, pengine ulipomwambia dada mdogo "kwa heri," au Baba, au baadhi yao kaburini, ukaahidi utakutana nao, na wewe—wewe hujafanya matayarisho hayo bado. Hivi hamfikiri ni wakati mzuri sasa wa kufanya jambo hilo?

Samahani kwa kububujika machozi. Lakini, loo, jamani, hutambui, rafiki. Hujui ni—ni dhabihu gani! Hiyo hata si hata nukta, moja ya hadithi ya hayo maisha, haifikii.

134 Ni wangapi wenu mngenda kuinuka sasa na kutembea kuja hapa kwa maombi, msemi, "Nataka kukutana na wapenzi wangu?" Simama utoke kwenye makutano uje hapa. Utafanya hivyo? Kama mtu fulani hajawahi kufanya matayarisho hayo bado. Mungu akubariki, bwana. Ninaona mzee mweusi akitokea, wengine wakija. Jisogeze mwenyewe, ninyi mlio kwenye rohani kule juu, tokeni tu moja kwa moja kwenye marefu ya kanisa. Ama simama, wewe unayetaka kukumbukwa katika neno la maombi sasa hivi. Hivyo ndivyo ilivyo. Simama moja kwa moja kwa miguu yako. Hilo ni jema. Simama, kila mahali, wewe ambaye ungesema, "Nina baba kule, nina mama ama mpendwa kule. Ninataka kwenda kuwaona. Ninataka kukutana nao kwa amani." Utasimama, simama tu kwa miguu yako, po pote katika kusanyiko. Simama kwa miguu yako, useme, "Ninataka kukubali."

135 Mungu akubariki, mama. Mungu akubariki huko nyuma. Na akubariki huko juu. Bwana akubariki hapa, bwana. Hiyo ni kweli. Huko juu kwenye rohani, Bwana awabariki. Kila mahali, kila mahali, simameni kwa miguu yenu sasa ili tuombe, wakati Roho Mtakatifu yuko hapa na akitembea mioyoni mwetu, ku—ku—kuivunjavunja.

Mwajua, kile kanisa linachohitaji leo ni kuvunjika. Tunahitaji kushuka kwenda kwenye Nyumba ya Mfinyanzi. Theolojia yetu ngumu ya kujitengenezea wakati mwingine haifanyi kazi vizuri sana. Tunachohitaji ni kuvunjika kwa mtindo wa kale, toba mioyoni mwetu, kuwa wasio wagumu mbele za Mungu. Hao tu sasa ndio walio tayari kusimama?

Hebu na tuinamishe vichwa vyetu basi kwa maombi.

136 Ee Bwana, uliyemleta tena Yesu kwa ajili ya ... kutoka kwa wafu, kutuhesabia haki sisi sote kwa imani, tukiamini. Ninaomba, Bwana, ya kwamba hawa wanaosimama sasa kwa miguu yao kukukubali Wewe, ninaomba ya kwamba msamaha utakuwa kwao. Na, Ee Bwana, ninaomba ya kwamba watakukubali kama Mwokozi wao na Mfalme na Mpenzi wao, na labda wana mama ama baba ama mtu fulani ng'ambo ya bahari. Kuna jambo moja la hakika, wao wana Mwokozi. Jalia wasamehewe dhambi zao, na uovu wao wote ufutiliwe mbali, ili kwamba nafsi zao zipate kuoshwa katika Damu ya Mwana-Kondoo, nao waishi kwa amani tangu sasa.

Na siku fulani yenye utukufu wakati yote yamekwisha, jalia tukusanyike kwenye Nyumba Yako, na tuwe pale kama familia zisizovunjika, kukutana na wapendwa wetu wanaongojea upande ule mwingine. Hawa, tunawakabidhi Kwako, ya kwamba "Wewe utamlinda katika amani kamilifu ambaye moyo wake umemtegemea." Tujalie, Bwana, tunapowakabidhi Kwako. Katika Jina la Mwanao, Bwana Yesu. Amina.

137 Mungu akubariki. Nina hakika watenda kazi wanaona mnaposimama, na watakuwa pamoja nanyi katika dakika chache.

Na sasa kwa wale ambao watakaopokea kadi za maombi. Billy, wako wapi Gene na Leo, wako kule nyuma? Wako hapa kutoa kadi za maombi katika dakika chache tu. Ndugu atawaruhusu watu wafumukane kwa maombi, na kadi za maombi zitatolewa. Tutarudi hapa punde tu, kuwaombea wagonjwa. Vema, ndugu.



www.messagehub.info

Mahubiri Na
William Marrion Branham
"... katika siku za sauti ..." Ufu. 10:7